**28 AGOSTI, 2026**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 28 Agosti, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:**

Maelezo ya Waziri wa Kilimo kuhusu Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026.

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Mheshimiwa Emmanuela Kaganda Mtatifikolo, Mbunge wa Isimani, sasa aulize swali lake.

Na. 28

### Barabara ya Itunundu – Izazi

**MHE. EMMANUELA K. MTATIFIKOLO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatenga fedha za kukamilisha ujenzi wa barabara ya Itunundu hadi Izazi yenye kilometa 45?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Jafar Rajab Seif, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuela Kaganda Mtatifikolo, Mbunge wa Jimbo la Ismani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara inayotoka Itunundu hadi Izazi ambayo ipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Jimbo la Isimani. Barabara hiyo ni muunganiko wa barabara tatu ambazo ni Izazi – Mboliboli (kilometa 26), Pawaga Sekondari – Mboliboli (kilometa 10) zinazosimamiwa na *TARURA* na sehemu iliyobakia ipo katika barabara ya Iringa – Pawaga inayosimamiwa na *TANROADS* - Iringa yenye urefu wa kilometa tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hizi zote ni muhimu kwani ni tegemeo kubwa kwa wakazi wa Tarafa ya Pawaga

ambao uchumi wao unategemea sana kilimo cha zao la mpunga. Mbali na shughuli za kiuchumi pia ni muhimu kwa mahitaji ya kijamii hususan sekta ya afya na elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kukamilisha barabara hizi ambapo mpaka sasa jumla ya kilometa 3.25 zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, kilometa 5.5 zinaendelea kujengwa ambapo wakandarasi wawili wapo eneo la mradi, ambao ni *NARMO Company Limited* anajenga kilometa 2.5 kwa jumla ya fedha za kitanzania shilingi bilioni 1.68 na *Chelesi Enterprises* anajenga kilometa 2.42 kwa jumla ya shilingi bilioni 1.72, ambapo ikikamilika jumla ya kilometa 8.25 zitakuwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha ili kuendelea kuikamilisha barabara hiyo kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuela Kaganda, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUELA K. MTATIFIKOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri lakini pia ninawashukuru kwa kuendelea kutenga fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imeshatoa fedha zaidi ya shilingi bilioni 56 na hivi karibuni tunatarajia kupata shilingi bilioni 36 kwa ajili ya kuimarisha skimu za umwagiliaji kwenye Bonde lile la Pawaga, kwa skimu moja ambayo tumeshapata shilingi bilioni 56 uzalishaji umeshaanza, skimu imeshakamilika na uzalishaji umeanza na uzalishaji umekuwa kwa kiasi kikubwa sana, changamoto ni barabara hiyo ya kuweza kupeleka mazao sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba majibu ya Serikali au ninauliza kwamba Serikali haioni haja ya kuweza kumalizia

barabara ile kwa wakati ili wananchi wetu wa Bonde la Pawaga waweze kufikisha mazao yao sokoni kwa urahisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninamuomba Mheshimiwa Naibu Waziri tuweze kuambatana kwenda Pawaga ili akaone kazi kubwa ambayo imefanywa na Serikali ya kusaidia uzalishaji wa mpunga kwenye bonde lile na changamoto kubwa ambayo wananchi wetu wanaipata katika kufikisha mazao yao sokoni kwa kukosekana kwa barabara hii. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Emmanuela Mtatifikolo, Mbunge wa Jimbo la Ismani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, amekuwa akifanya ufuatiliaji wa miradi mbalimbali katika Jimbo la Ismani na wana-Ismani ninawahakikishia mmepata mwakilishi ambaye anawasemea nyakati zote hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina miradi mbalimbali katika tarafa hii kwa wananchi hawa wa Pawaga na miradi mingi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alielekeza kule ili kuongeza uzalishaji wa zao letu la mpunga. Sisi kama *TARURA* hatuwezi kuwa kikwazo, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Profesa Riziki Shemdoe amekwishaelekeza fedha na amekwishaelekeza wataalam kuhakikisha kwamba ujenzi wa kilometa 5.5 unaendelea. Mpaka sasa wakandarasi wapo *site* na kile kipande kingine ambacho kinabakia cha changarawe tunakirekebisha ili kiweze kupitika nyakati zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, zile kilometa tisa ambazo zipo chini ya *TANROADS* ninawasiliana na wenzetu wa ujenzi ili waweze kuzijenga na tupate muunganiko huo ili kuweza kurahisisha usafirishaji wa mazao katika Jimbo letu hili la Ismani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; tumekuwa tukifanya ziara, na ziara yangu ya kwanza nilianzia katika mikoa hii ya Nyanda za Juu Kusini, nilifika katika Halmashauri za Iringa. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutakwenda baada ya Bunge hili Tukufu, tutaongozana mimi na yeye twende tukawatie moyo wananchi kuongeza uzalishaji lakini kuhakikisha kwamba tunachagiza shughuli za maendeleo na kuhakikisha kwamba barabara hizi tunazifikia na kuelekeza ujenzi unaoendelea ufanyike kwa wakati na itoe huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Sibwesa – Katuma ni barabara ambayo imeharibika baada ya mvua nyingi kunyesha. Ni lini Serikali itaenda kukarabati hiyo barabara sambamba na kujenga madaraja ambayo yameharibika kwenye barabara hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakumbuka Bunge lako Tukufu lilituidhinishia bajeti na namna ya fedha ambazo tunaziongeza kule *TARURA* na uwezekano wa fedha ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu jana alipokuwa akijibu maswali hapa Bungeni aliishukuru Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba zile fedha sasa haziendi Hazina zinakwenda moja kwa moja kwenye Mfuko wa *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Kakoso kwamba tunaendelea kuratibu barabara hizo na kuhakikisha kwamba tunazijenga na kurekebisha miundombinu ya madaraja ili yaendelee kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninapenda kuipongeza Serikali kwa kutuletea miradi ya barabara za *DMDP* katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam na hususan katika Jimbo langu la Temeke, barabara hizo mpaka sasa wakandarasi bado wanasuasua. Maeneo mengine kama Kata ya Kurasini wamemwaga vifusi huu sasa karibu ni mwaka mzima na hakuna kinachoendelea.

Je, Serikali mnatoa kauli gani kwa wakandarasi hao ambao mpaka sasa hivi wanasuasua kuendeleza barabara zetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama alivyoliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyowapambania wananchi wa Jimbo la Temeke, kupitia Bunge lako Tukufu ninamuelekeza Meneja wa *TARURA* Mkoa na kushirikiana na Meneja wa *TARURA* Wilaya wafike eneo la tukio kusisitiza wakandarasi wetu waendelee kufanya jitihada za kuhakikisha kwamba barabara hizi wanazijenga kwa wakati na kusambaza vifusi ambavyo vinaleta adha kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawahakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na wana-Jimbo la Temeke kwamba barabara hizi tutazirekebisha kwa wakati ili ziendelee kutoa huduma. Ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakulu Kakulu, swali la nyongeza.

**MHE. KAKULU B. KAKULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa nafasi. Swali ninalokusudia kuuliza kwa Serikali linakaribiana kufanana na la Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba programu za uendelezaji wa Mji wa Dar es Salaam hasa zile barabara zinazoendelezwa kwenye Jimbo langu, barabara ya Kipati, barabara ya Kilimahewa, barabara ya Masuliza bado fidia haijakamilika na kwa hiyo wakandarasi wakati mwingine wanasuasua na kuleta visingizio.

Je, Mheshimiwa Waziri na Serikali wapo tayari kutembelea miradi hii kwa pamoja ili tuweze kuweka msukumo na *speed* iweze kuongezeka? Kwa vile tunatarajia mvua nyingi zinaweza zikaja hivi karibuni tusipofanya jitihada mapema tunaweza tukasababisha hasara kubwa sana kwa Serikali. Kwa hiyo, ninapenda kuwaomba kama mtakuwa tayari tutembelee miradi hiyo. Ninashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali na ombi la kutembelea miradi hii ili kuhakikisha kwamba inakamilishwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tumesimama kidogo kutangaza tenda na kutangaza barabara hizi na kuzitengea fedha lakini sasa tayari mifumo ishafunguka tumeruhusu fedha zishuke na kuanza kupeleka wakandarasi wetu ili waweze kurekebisha barabara hizi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutatembelea miradi na barabara ambazo amezielekeza hapa ili tuweze kuwaamsha wakandarasi wetu na kuwasisitiza ili waweze kuzijenga kwa wakati kuliko kupoteza zile fedha nyingi ambazo tumewekeza kwenye barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mheshimiwa Regina Henry Mikenze, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 29

**Uhamisho kwa Watumishi wanaofanyakazi mbali na Wenza Wao**

**MHE. REGINA H. MIKENZE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwahamisha watumishi wenye ndoa zinazotambulika kisheria kukaa karibu na wenza wao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Regina Ndege, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Regina Henry Mikenze kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upangaji wa watumishi wa umma baada ya kuajiriwa huzingatia vigezo mbalimbali ikiwemo maslahi ya kifamilia, mahitaji ya kisekta, ujuzi wa mtumishi na usawa wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa watumishi wa umma kuishi pamoja na wenza wao kama msingi wa kuimarisha familia na kuongeza ufanisi wa kiutendaji, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo, kuweka dirisha mahsusi kwenye mfumo wa *e-Utendaji* ambapo watumishi wa umma wanaomba kuhama kwa sababu nyingine ikiwemo kuwafuata wenza wao. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 watumishi 460 wakiwemo wanawake 281 na wanaume 179 walihamishiwa sehemu mbalimbali ili kuungana na wenza wao wa ndoa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Regina Henry, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA H. MIKENZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa maswali ya nyongeza. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa lakini bado ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kufahamu ni kweli mfumo unaweza ukawajibu watu wanaoomba uhamisho kwamba nafasi zimejaa lakini sisi kama binadamu tunazo changamoto mbalimbali za kibinadamu, kuna watu ambao wana matatizo yasiyoweza kuzuilika kwa mfano, wagonjwa ambao wanahitaji kuwa karibu na hospitali ili kupatiwa matibabu kwa haraka na kwa ukaribu, wanapoingia kwenye mfumo halafu wakaambiwa hakuna nafasi, nafasi zimejaa.

Je, Serikali inaweza kuwasaidiaje watu ambao wana changamoto kubwa kama hizo? *(Makofi)*

Swali la pili, wapo waajiri ambao wamekuwa wakiwakatalia waajiriwa wao wanapoomba uhamisho katika ngazi ya mwanzo

kabisa, ambapo wanatakiwa kuwajazia ili wao waendelee mbele na mfumo lakini wanazuiliwa na waajiri wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kufahamu, Serikali ina majibu gani kuhusiana na waajiri kama hao wanaowazuia waajiriwa wao? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri ya nyongeza lakini ninampongeza kwa namna ambavyo ameendelea kuwasemea watumishi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mkakati na miongozo mbalimbali inayowezesha watumishi wa umma kuweza kuomba uhamisho ili kufuata wenza wao. Katika mikakati hiyo ni pamoja na kuanzisha mfumo wa kielektroniki unaotambulika kama *e-Uhamisho* ambao unamuwezesha mtumishi kuomba uhamisho au kuwasilisha ombi lake la uhamisho kwenye mfumo ili aweze kumfuata mwenza wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo Serikali imeendelea kutazama kwa karibu, pamoja na kwamba mtumishi anapoingia kwenye mfumo, mfumo unaweza ukamkatalia kwamba nafasi hakuna au hajatimiza vigezo, Serikali kwa kuzingatia kauli ya Mheshimiwa Rais ya kusema Kazi na Utu, tumeendelea kuwaangalia kwa karibu watu wote ambao wana uhitaji maalum hususan wagonjwa, tumeendelea kuwapa nafasi hiyo ya uhamisho ili kuweza kuungana na wenza wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha pili ambacho amesema Mheshimiwa Mbunge kwamba wapo waajiri ambao kwa namna moja ama nyingine wanakataa kupitisha uhamisho. Serikali imeendelea kutoa miongozo mbalimbali kwa waajiri wote nchini. Kwanza kuhakikisha kwamba wanatatua changamoto za watumishi kwa haraka lakini kushughulikia masuala yanayohusu uhamisho kwa wepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora niendelee kuwakumbusha waajiri wote nchini kuhakikisha kwamba masuala yote ya kiutumishi yanashughulikiwa kwa wakati, hususan masuala yanayohusu uhamisho. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaipongeza Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan na Wizara yenu ikiongozwa na Waziri, Mheshimiwa Ridhiwani, kwa kazi nzuri ambazo mnafanya na matatizo ya watumishi yameanza kupungua. Hata hivyo, kumekuwa kuna changamoto pale watumishi wanapohamishwa kuchelewa kulipwa pesa zao za mizigo.

Nini mkakati wa Serikali kushughulikia matatizo haya ya watumishi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Ester Bulaya kwa swali lake zuri lakini kwa kuendelea kuwasemea watumishi na mara zote tumeona namna ambavyo amesimama hapa na kusemea watumishi katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Serikali ni kwanza uhamisho unapotolewa ni pale ambapo Serikali imejiridhisha imetenga bajeti kwa ajili ya kuwahamisha hao watumishi. Wakati mwingine ni kweli uhamisho umetoka na mtumishi hajalipwa kwa wakati huo. Serikali imeendelea kutoa miongozo mbalimbali kwa waajiri wote katika maeneo yote kuanzia Halmashauri na

kuendelea, kuhakikisha wanapomhamisha mtumishi lazima wawe wametenga bajeti ya kumlipa yule mtumishi pindi anapohama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama mtumishi amehamishwa tunapenda kuendelea kuwakumbusha waajiri wote kuhakikisha kwamba watumishi wote wanalipwa kwa haraka pale ambapo uhamisho umetolewa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Mwanaenzi Hassan Suluhu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 30

**Idadi ya Vijana waliowezeshwa kupitia Programu za Uwezeshaji**

**MHE. MWANAENZI HASSAN SULUHU** aliuliza:-

Je, vijana wangapi wamewezeshwa kupitia programu za uwezeshaji kwa kipindi cha miaka mitano na matokeo yake katika kupunguza tatizo la ajira?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanaenzi Hassan Suluhu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano kuanzia Julai, 2021 hadi Juni, 2026 jumla ya vijana 1,373,433 wamewezeshwa kupitia programu mbalimbali zinazotekelezwa

na Serikali, taasisi za umma, sekta binafsi na wadau wa maendeleo. Uwezeshaji huo umehusisha mikopo na mitaji, mafunzo ya ujuzi, uanagenzi, *internship*, uzoefu kazini, pamoja na fursa katika sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, biashara, viwanda vidogo, utalii, teknolojia, sanaa na uchumi wa kidijitali. Aidha, vijana wameunganishwa na ajira, zabuni za umma, masoko na huduma za ukuzaji biashara na ujasiriamali. Hatua hizi zimeongeza uwezo wa vijana kuajirika, kujiajiri lakini pia kuanzisha biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hizi ni za awali na zinaweza kuongezeka kutokana na baadhi ya programu kutoripotiwa kwa wakati, kwa kuwa hakukuwa na mfumo mmoja wa kitaifa wa kuratibu na kukusanya takwimu za wanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto hiyo, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana imekamilisha hatua ya kwanza ya ujenzi wa mfumo wa kisasa wa uwezeshaji vijana na inaendelea na hatua ya pili, sambamba na kukamilisha mfumo wa kitaifa wa uratibu wa masuala ya vijana. Mifumo hiyo itaimarisha usajili wa wanufaika, ukusanyaji na uhakiki wa takwimu, lakini pia uratibu wa programu na ufuatiliaji wa matokeo ya uwezeshaji wa vijana nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwanaenzi Hassan Suluhu, swali la nyongeza.

**MHE. MWANAENZI HASSAN SULUHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu hayo mazuri ya Serikali.

Je, ni vijana wangapi kati ya hao ambao kwa sasa wanayo ajira ama wameweza kuanzisha shughuli endelevu za kujiajiri?

Je, ni upi mkakati wa Serikali kwa vijana ambao hawajafanikiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Mwanaenzi kwa kuendelea kufuatilia masuala yanayohusiana na vijana na ustawi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano inayokuja tumeweka mkakati kama Serikali wa kuzalisha ajira takribani milioni 8.5. Utekelezaji wa mpango huu umeanza mwezi Julai mwaka huu. Ningependa kumuomba Mheshimiwa Mbunge, kwamba tutamletea taarifa za kimaandishi zinazoonesha idadi ya vijana ambao wamepata ajira kutokana na uwezashaji huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba vijana wa Taifa letu wanapata fursa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya fursa ambayo Mheshimiwa Rais aliitoa ni kupitia bajeti iliyopita ya kwamba vijana au Watanzania watapewa *grace period* ya miezi 12 kabla hajaanzisha biashara. Kwamba, akianzisha biashara miezi 12 watafanya *for free* baadaye ndipo atakapoanza kulipa kodi.

Ninataka kufahamu, Je, huo mkakati umeanza au bado?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Festo Sanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliahidi, eneo mojawapo ambalo aliwekea mkazo zaidi ni kutengeneza mazingira bora hasa katika uwezeshaji wa vijana. Katika hilo, yako mambo ambayo aliyasema yafanyike, mojawapo ilikuwa ni kutoa unafuu kwa vijana ambao wanaanza biashara ili kuwapa muda wa kukuza biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na swali alilouliza ningetangulia kusema kwamba, eneo mojawapo ambalo alielekeza na tumeanza kulifanyia kazi ni vijana kupata *grace period* wanapopata mikopo inayotolewa na taasisi za Serikali. Katika hili wanapata miezi mitatu kwa biashara ambazo ni za kawaida lakini biashara zinazohusiana na kilimo na mifugo huwa tunawapa muda wote mpaka watakapokuwa wamefanya mavuno yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tulipitisha hapa Bungeni na ningependa kukutaarifa kwamba sheria hii imeanza kutekelezwa na vijana ambao wanaanzisha biashara kwa sasa wanapata unafuu wa mwaka mmoja bila kulipa kodi ili kuruhusu biashara zao zikue na waweze pia kujijenga kiuchumi zaidi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kuweza kunipatia fursa ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi za Serikali, ambazo tunazipongeza za kuongeza ajira, ninataka kujua ni mikakati gani mahsusi na yakupimika ambayo Serikali wameweka ili kuhakikisha kwamba vijana hasa waliomaliza vyuo na vyuo vikuu wanaweza kupata ujuzi, mitaji na masoko ili sasa waweze kubadili ujuzi walio nao walioupata kwenye vyuo na vyuo vikuu kugeuza kuwa fursa za kiuchumi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Matiko kwa kuuliza swali hilo zuri na kuendelea kufuatilia pia ustawi wa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tuliweka mkakati katika uzalishaji wa ajira katika miaka mitano ijayo 55.1% itatoka kwenye eneo la kilimo, ambayo inajumuisha pia ufugaji lakini pia inajumuisha mazao ya misitu. Asilimia 32.7 tumesema yatatoka

katika sekta ya *SMES* biashara ndongo na pamoja na kati na 12.3% itatoka katika sekta ambayo ni rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba jambo hili linatekelezeka sisi kama Wizara tumetengeneza mpango maalum ambao unahusisha ufuatiliaji na pia tathmini, sawasawa na maelekezo ya utekelezaji wa Dira ya mwaka 2030, ambayo katika *instruments* ambazo Mheshimiwa Rais alizindua mojawapo ilikuwa ni eneo la ufuatiliaji. Sisi kama Wizara tayari tumekwishatengeneza mpango wa ufuatiliajia ambao unaweza ukaonesha katika kila sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo mojawapo ni vijana wanaomaliza vyuo vikuu. Kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Ajira pamoja na mahusiano hasa katika kuwaandaa vijana kupitia programu maalum tunaendesha programu za kuwasaidia kufanya mojawapo ni kuangalia mahitaji halisi yaliyopo katika soko la ajira kwa maana wanahitaji nini. Kwa hiyo, tunao mkataba maalum wa sekta binafsi na Serikali ambao pia tunawapa nafasi ya kufanya mazoezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali inatenga fedha kila mwaka kuhakikisha kwamba vijana wanapata nafasi ya kwenda kufanya majaribio na wanalipwa na Serikali wanapokuwa wanakwenda kule kama njia pia ya kuongezea ujuzi wao.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Afya, ninamwita Mheshimiwa Asma Ali Mwinyi sasa aulize swali lake.

Na. 31

**Usambazaji wa Huduma za *ORCI* Mikoani**

**MHE. ASMA ALI MWINYI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza huduma za *ORCI* mikoani ili kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya *Ocean Road?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Asma Ali Mwinyi, Mbunge wa Welezo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa huduma za matibabu ya saratani zinapatikana nchi nzima na kuwapunguzia wananchi umbali wa kufuata huduma, Serikali inatekeleza ujenzi wa mradi wa matibabu ya Saratani katika Hospitali za Kanda za Benjamini Mkapa, ambapo mradi umefikia asilimia 80 kwa gharama ya shilingi bilioni 28.9 na Hospitali ya Kanda Mbeya ambapo ujenzi umefikia asilimia 60 kwa gharama ya shilingi bilioni 10. Miradi hii inatarajiwa kukamilika Januari, 2027. Aidha, Serikali imetoa shilingi bilioni 5.3 kwa ajili ya ujenzi wa *bunkers* za mashine za mionzi katika Hospitali za Kanda za *KCMC* na Bugando ambapo huduma zimeshaanza na kuzifanya hospitali hizi kuwa na uwezo timilifu wa kutoa tiba mionzi na dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imepiga hatua kubwa kwa kuviwezesha vituo vya kutolea huduma zaidi ya 1,760 kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali ya Taifa kuchunguza na kutoa matibabu ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asma Ali Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. ASMA ALI MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ambayo nimepata kutoka kwa Serikali. Ninaomba niulize maswali mawili.

Swali langu la kwanza ni kwamba Serikali imetaja kwamba imeongeza huduma za saratani katika hospitali za kanda. Je, ni lini huduma hizi zitaanza kikamilifu Zanzibar ili kupunguza idadi ya watu ambao wanasubiri kufika *Ocean Road?*

Swali langu la pili, kwa kuwa Serikali imeeleza kwamba imewekeza *heavily* katika hospitali za Kanda, ningependa kujua Serikali ina mkakati gani mahsusi wa kuweza kupima kujua huu msongamano na huduma za kusubiria watu kufika umepungua kwa idadi gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Asma kwa kuendelea kuwapigania wananchi wa Tanzania, hasa wagonjwa wa ugonjwa huu wa saratani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliandaa andiko la uwekezaji wa huduma timilifu ikishirikiana na Serikali ya Zanzibar na kutumia Tume ya Atomiki, na ilipanga kufanya uendelezo wa kufanya huduma timilifu Tanzania Bara na Zanzibar. Hospitali ya Binguni Zanzibar nayo iko kwenye uendelezo wa kufanya huduma timilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, ndani ya miaka miwili kwa maana ya kuanzia sasa Zanzibar nayo itapata huduma timilifu ya mionzi kwa sababu tunashirikiana katika kutoa huduma hizo. Hata sasa wagonjwa ambao hawapati huduma timilifu wanapata huduma hizo katika hospitali yetu ya *Ocean Road.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili, tayari Serikali imekwishaona manufaa ya kusambaza huduma hizi katika hospitali za mionzi za kanda kwa sababu awali wagonjwa hawa walikuwa wanasubiri huduma za matibabu kwa wiki 16, lakini mpaka sasa hivi wagonjwa hawa wanasubiri huduma za kimatibabu kwa wiki saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, kwa kupungua muda wa kusubiri kuanza mionzi kutoka hii 16 mpaka saba tayari uwekezaji uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita umekwishaleta manufaa makubwa. Hata hivyo, wananchi mwendo wa kufuata huduma umepungua kwa sababu wale wote waliokuwa wanakuja *Ocean Road* wanapata huduma hizi Bugando, wanapata huduma hizi *KCMC,* kwa hivyo sasa hawasafiri mwendo mrefu. Wale wanaokuja *Ocean Road* ni wale wanaohitaji huduma za kibingwa na kibingwa bobezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge ninaomba tujadili mambo yetu kwa sauti ya chini ili Waziri anapojibu asikike na muuliza swali pia asikike. Mheshimiwa Adonis Bitegeko, kwa swali la nyongeza.

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya changamoto kubwa ya wagonjwa wa *cancer* hasa wanatokea vijijini ni kuwa na elimu ndogo ya uelewa kuhusu ugonjwa huo lakini pia kumudu gharama ya uchunguzi na matibabu.

Je, Serikali imejipanga vipi katika kuweza kuwawezesha wananchi kielimu lakini pia kuwezesha katika gharama za matibabu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Watanzania wote wanahitaji elimu ya kutosha kuhusiana na namna ya kujikinga na magonjwa haya ya saratani pamoja na jinsi ya kutambua mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inayo mpango maalum wa kutoa elimu ya afya kupita vyombo vya habari, kupitia *page* zote za Wizara lakini na wataalamu katika ngazi ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika swali la awali, kwamba vituo 1,760 katika ngazi ya msingi vina uwezo wa kugundua magonjwa haya na kutoa elimu. Kwa hivyo, kupitia njia hiyo tunatoa elimu. Pia, Serikali inao utaratibu wa kufanya kliniki, kwa maana ya *MKOBA outreach* ambazo hizi nazo hutumika kufanya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nanyi mmekuwa mashuhuda hata katika matukio ya kawaida ya kitaifa tunaendelea kutoa elimu ya jinsi gani ya kutambua madhara haya ya saratani ili wananchi waweze kutambua mapema kwa sababu wakitambua mapema basi ugonjwa huo unatibika. Vilevile tunaendelea kutoa elimu ya kujikinga kwa sababu magonjwa haya pale ambapo tutachukua tahadhari ya yale mambo ya visababishi ambavyo vinakupelekea kuwa na uhatarishi wa kupata *cancer* basi *chance* ya kupata saratani inakuwa ndogo. Hivyo, ni mkakati endelevu na Serikali tumejipanga kuendelea kutoa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, sasa ulize swali lake.

Na. 32

**Changamoto ya Upatikanaji wa Visa kwa Watanzania wanaofuata bidhaa China**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza:-

Je, Serikali inaweza kufanya majadiliano na Serikali ya China kurahisisha upatikanaji wa *visa* kwa Watanzania wanaofuata bidhaa China?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afirika Mashariki, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. DKT. NGWARU J. MAGHEMBE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abbas Gulam Tarimba, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya majadiliano ya mara kwa mara na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa *visa* hapa nchini kwa kutoa kipaumbele kwa wafanyabiashara, kwa kuwapatia visa za muda mrefu zinazowaruhusu kuingia China mara kwa mara *(multiple entry viza)*. Mathalan, mwezi Julai, 2026 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikutana na Balozi wa China na kuwasilisha ombi kuhusu uwezekano wa kutoa viza za muda mrefu kwa Watanzania, hususan wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ya China ililifanyia kazi ombi la Mheshimiwa Rais na kuongeza idadi ya visa zinazoruhusu wafanyabiashara kuingia mara kwa mara nchini China na hivyo kupunguza hitaji la kuomba visa kila wanapotaka kusafiri kwenda nchini humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Serikali ya China imeahidi kuanzisha Kituo Maalumu cha Maombi ya Visa *(China Visa Application Centre)* Jijini Dar es Salaam ili kuhudumia Watanzania kwa urahisi tofauti na hivi sasa ambapo masauala ya visa yanafanyiwa kazi na Ubalozi wa China pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana. Ninaishukuru na kuipongeza Serikali kwa juhudi zake kuweza kuwasaidia watanzania kuweza kuondokana na urasimu mkubwa ulipo katika Ubalozi wa China.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ndiyo wapo watu wanaokata *visa* za muda mrefu, lakini watanzania wa kawaida wenye *pass* za kawaida, siyo hizi za kidiplomasia wala hizi za kiutumishi, hulazimika wengine kwenda usiku kupanga foleni kusubiri muda wa kuingia ubalozini. Watanzania hao ndiyo wanaotuletea bidhaa nyingi kutoka China kiasi kwamba Serikali inapata kodi kubwa kutokana na shughuli hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la nyongeza, kwa kuwa Wachina wanapokuja Tanzania wanapata *visa on arrival* wakifika pale Tanzania mpakani wanagongewa wao hawasoti kwao kuomba *visa* ya kuja Tanzania.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba Serikali inahitaji sasa kufanya mazungumzo na Serikali ya China kuwa na mkataba wa *reciprocal agreement*, kwa maana ya watanzania wanapofika China nao waweze kupata *visa on arrival?*

Swali langu la pili, ili kuweza kusubiri huo muda wa majadiliano, je, Serikali haioni haja sasa ya kuongea na Serikali ya China kupunguza urasimu wa mahitaji ya Mtanzania kupeleka kwenye Ubalozi ili *visa* zile ziweze kupatikana na kufungua fursa zaidi kwa watanzania kwenda kufanya biashara China?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. DKT. NGWARU J. MAGHEMBE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kwanza kabisa ningependa kumpongeza Kaka yangu Mheshimiwa Tarimba kwa kuuliza swali zuri na kwa niaba ya sekta binafsi yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba Tanzania na China tunayo mahusiano mazuri sana ya kiundugu, lakini pia ya kibiashara. Hapa tulipo sasa hivi kila mwaka thamani ya biashara kati ya China na Tanzania ni Dola za Kimarekani bilioni tisa na bidhaa zinazouzwa hapa nchini Tanzania 28% zinatoka China. Kwa hiyo, ninaielewa vizuri *concern* ya Mheshimiwa Tarimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *visa on arrival* ni kweli kabisa kwa sasa watanzania ambao wana *diplomatic passport* kama ninyi Waheshimiwa Wabunge na Watanzania ambao wana *service passport* zile *passport* za huduma wao tu ndiyo wanaweza kupata *visa on arrival in China*. Watanzania walio wengi wao ni lazima kwanza wa *apply* hapa nyumbani, wakipata hapa ndipo wasafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hii Serikali ilikuwa imekwishaiona tangu mwishoni mwa mwaka jana, Januari mwaka huu 2026 alivyokuja Mjumbe wa Kamati Kuu na Waziri wa Mambo ya Nje wa China Mheshimiwa Wang Yi, Serikali kupitia Waziri wetu wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Balozi Mahmoud Thabit Kombo ilipeleka ombi lao rasmi, kwamba sasa jamani na sisi watanzania ndugu zenu tuweze kupata *visa* zetu tukiwa tunafika hapo Shanghai au Beijing.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba hili ombi limepokelewa vizuri na ndugu zetu wa China na wanaendelea kulichakata. Kwa hatua ya awali wametuahidi haraka iwezekanavyo wataanzisha *visa application centre* Dar es Salaam lakini pia na Mjini Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea na nimepokea sana kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri na Wizara yetu kwamba tumepokea hii *push* ya kwake Mheshimiwa Mbunge na tutaendelea kulifuatilia kwa ukaribu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili ambalo sasa, jamani wakati tunasubiri tunayo mikakati gani Wizara mmefanya. Ninashukuru sana kwa hili swali, Wizara tumekuwa tunafanya

majadiliano ya mara kwa mara na ndugu zetu Ubalozini China na tumekubaliana vitu vitatu. Kwanza, tumekubaliana na wameshaanza kutekeleza ni kwamba waongeze ufanisi kwenye *process* ya *visa.* Wameshaongeza idadi ya *staff* kwenye *visa section* yao na pia wamewaongezea muda wa kufanyia kazi. Walikuwa wanafanya kazi kuanzia Saa Mbili Asubuhi mpaka Saa Nane, sasa hivi wanafanya kazi kuanzia saa 2.00 asubuhi mpaka saa 11 jioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, ni hili ambalo nimesema kwenye jibu langu la msingi kwamba mwenye mamlaka mwenyewe, Mheshimiwa Rais amewaomba Balozi na Serikali ya China kwamba jamani, hawa wafanyabiashara ambao wanaenda mara kwa mara, mtu anaenda mara nne, mara tano, kwa nini aombe *visa* mara nne, mara tano au mara sita? Ni afadhali apewe *multi-entry visa* na hili ombi limeshakubaliwa na linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, Kaka yangu, *my senior brother* Mheshimiwa Tarimba ni kwamba, tumekubaliana na Balozi na Wizara kwamba tutatoa elimu kwa umma kwamba jamani hivi ndiyo vitu vinavyohitajika ukiwa unahitaji *passport*, hiyo utapunguza ile nenda, rudi, umesahau hiki, umesahau hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kupitia Bunge lako Tukufu na hawa Wabunge wazito ninaomba niwaelimishe au niwaombe wananchi wetu wa Tanzania kwamba tunaomba mkiwa mnaomba *visa* za China mpeleke maombi yenu wiki tatu kabla ya siku ambayo unasafiri, mkifanya hivyo mimi ninawahakikishia kwamba mtakuwa mnapata *visa* zenu mapema bila kukosa safari zenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 33

**Kujenga upya Makazi ya Askari Polisi – Mbulu**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga upya makazi ya askari polisi Wilayani Mbulu kwa kuwa yaliyopo ni chakavu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kujenga na kufanya ukarabati wa nyumba za makazi ya askari polisi ili kuongeza ari ya kutoa huduma bora ya ulinzi na usalama kwa wananchi. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeandaa mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Jeshi kwa kipindi cha miaka mitano 2026 - 2031. Hivyo, ujenzi wa nyumba za makazi ya askari polisi Mbulu utakuwa katika mpango huo na unategemewa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2027/2028. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwa kuwa Wilaya ya Mbulu ni Wilaya kongwe nchini na kwa kuwa, makazi ya Askari katika Wilaya hiyo ni chakavu sana.

Je, Serikali iko tayari sasa kuweka kipaumbele katika mpango huu wa utekelezaji wa makazi ya Askari nchini?

Swali la pili, kwa kuwa Tarafa ya Nambis na Tarafa ya Daudi katika Mji wa Mbulu na Halmashauri ya Mji wa Mbulu hakuna vituo vya polisi. Je, mpango wa Serikali ukoje kujenga vituo vya Polisi katika Tarafa hizo mbili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu yangu ya msingi, Jeshi la Polisi Tanzania linao mpango wa kujenga makazi ya Askari, vituo vya Polisi lakini pia kukarabati maeneo ambayo nyumba zimechakaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huo kwa swali lake la msingi la kwanza, wananchi wa Mbulu na maeneo mengine kwa Tanzania mpaka sasa tumekwishajenga ofisi za daraja 'A' saba lakini pia daraja 'B' 16 na daraja 'C' 26. Pia, maeneo mengi hapa nchini tumekwishaanza utaratibu huo wa kufanya ujenzi na tumezingatia kuweza kufanya *assessment* na *need assessment* ya kila maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika huu mpango wa miaka mitano ambao tunao wa kuanzia mwaka wa fedha 2026/2027 hadi mwaka 2030/2031, tutakuwa tayari tumekwisha kufikia maeneo mengi. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo tutalizingatia na tutaendelea kuliweka kwenye bajeti kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mbunge wa Chambani, sasa aulize swali lake.

Na. 34

**Hitaji la Jengo la Ofisi ya *NIDA* Wilaya ya Mkoani – Kusini Pemba**

**MHE. MOHAMED ABDULRAHMAN MWINYI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga jengo la Ofisi ya *NIDA* la Wilaya ya Mkoani katika Mkoa wa Kusini Pemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mbunge wa Jimbo la Chambani, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na majengo ya ofisi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya usajili na utambuzi katika Wilaya za Tanzania Bara na Zanzibar. Kutokana na umuhimu huo, Serikali kupitia *NIDA* imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha uwepo wa majengo kwa ajili ya ofisi za usajili na utambuzi. Mikakati hiyo ni pamoja na kufanya mazungumzo na wadau wa maendeleo pamoja na kutenga fedha za ndani kupitia bajeti ya *NIDA* ili kujenga ofisi za usajili na utambuzi katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2027/2028 Serikali inatarajia kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya ofisi za usajili na utambuzi ikiwemo ofisi ya usajili ya Wilaya ya Mkoani - Kusini Pemba, kulingana na upatikanaji wa fedha na vipaumbele vya Mamlaka. Aidha, kukamilika kwa ujenzi wa ofisi hizo kutaboresha na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za usajili na utambuzi wa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED ABDULRAHMAN MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ofisi ya *NIDA* Wilaya ya Mkoani ni chumba kimoja tu na ni kidogo hakina nafasi, na kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani ina jengo ambalo walikuwa wanatumia Mahakama ya Wilaya na sasa hivi wameondoka.

Je, Serikali haioni haja ya kwenda kuazima jengo hilo ili wahamie kwa muda mpaka watakapojenga? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa *concern* hiyo aliyoi-*raise* Mheshimiwa Mbunge Mohamed Abdulrahman Mwinyi, ninaomba niseme kwamba nitatuma Maafisa kule waweze kufanya *assessment* ya kile alichokisema ili tuweze kuona tunaweza kulitekeleza kwa namna gani ili wananchi waweze kupata huduma hiyo inayostahili. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, swali la Mheshimiwa Mary Francis Masanja, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Regina Malima.

Na. 35

**Ukamilishaji wa Ujenzi wa *SGR* Dodoma – Mwanza**

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA K.n.y. MHE. MARY F. MASANJA** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa *SGR* Dodoma - Mwanza utakamilika ili kurahisisha huduma ya usafiri katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Tabora na Kanda ya Ziwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania *(TRC),* imeendelea na ujenzi na uendeshaji wa reli mpya ya *Standard Gauge Railway* (*SGR*). Ujenzi wa reli ya *SGR* unatekelezwa kwa awamu mbili, ikihusisha kilometa 1,219 za njia kuu kwa awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam – Mwanza na kilometa 1,590 za awamu ya pili ikijumuisha Tabora – Kigoma na kutoka Uvinza – Msongati. Aidha, kukamilika kwa awamu hizo mbili za reli ya *SGR* kutaifanya Tanzania kuwa na mtandao wa jumla ya kilometa 2,809 za reli ya kisasa ya *SGR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa *Standard Gauge Railway* (*SGR*) nchini katika kipande cha tatu, nne na tano unaendelea vizuri na upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, Serikali imeweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kipande cha kutoka Makutupora - Tabora hadi Isaka vinakamilika kwa wakati ikiwemo kumruhusu mkandarasi kutoa baadhi ya kazi kwa wakandarasi wengine *(sub-contractors)* pamoja na kuendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatarajiwa kwamba ifikapo mwaka 2030 ujenzi wa miundombinu ya *SGR* utakuwa umekamilika hadi Mwanza na kuanza uendeshaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Regina Malima, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kuanzisha huduma za treni za *SGR* kwenye *route* za Dar es Salaam - Dodoma na zimeonesha mafanikio makubwa katika kurahisisha usafiri kwa wananchi.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanza kutoa huduma za *SGR* kwa vipande vipande nikiwa na maana ya Dar es Salaam - Tabora, Tabora - Shinyanga kabla ya kukamilika kwa *route* nzima ya Dodoma - Mwanza ili wananchi wa Mkoa wa Tabora, Shinyanga na Kanda ya Ziwa kwa ujumla waanze kunufaika na huduma hiyo mapema? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa ujenzi wa bandari kavu katika eneo la Usagara Mkoani Mwanza ni muhimu katika kuimarisha usafiri wa mizigo lakini pia kupunguza gharama za usafirishaji na kuifanya Mwanza kuwa kitovu cha biashara katika Kanda ya Ziwa.

Je, ni lini ujenzi huo utaanza rasmi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa kwa swali ambalo ameuliza kwa niaba ya Mheshimiwa Mary Masanja na maswali yake yote mawili. Hata hivyo, ndani ya maswali yake amejawa na shukrani ya kazi ambayo inaendelea kufanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kwamba anakwenda kutimiza ajenda ya kuifikisha reli ya kisasa katika Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza ameleta kama ushauri kwamba, Serikali tusisubiri mpaka tukamilishe vipande vyote ndiyo tuanze utekelezaji. Ushauri huo umepokelewa na tumekwishaanza kutekeleza kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma kabla hatujaingia Mwanza wala kabla hatujaingia Kigoma. Kwa hiyo, tunaupokea kwa mikono miwili ushauri huu mzuri ambao ameutoa Mheshimiwa Mbunge ametimiza jukumu lake la msingi kabisa ambapo Bunge kazi yake pia ni kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili anahitaji kufahamu Bandari yetu ya Fela ni lini itaanza kujengwa kwa sababu bandari hii ni muhimu? Hili nalo ni swali zuri ambalo linajali tija ya usafirishaji wa mizigo kutoka Dar es Salaam kwenda moja kwa moja mpaka Mwanza. Nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii tayari imekwishaanza taratibu, kwanza kwa kutambua jambo hilo muhimu imetenga eneo la Fela.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuzingatia umuhimu wake hivi ninavyozungumza tumekwishaajiri mkandarasi, ni wiki iliyopita tu Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa Mbarawa ametoka kuwakumbusha wenzetu Mamlaka ya Bandari Tanzania kwamba anahitaji mkandarasi huyu akamilishe kazi mapema iwezekanavyo, ikiwezekana kabla ya Disemba ili baada ya kukamilika kwa usanifu wa kina pamoja na upembuzi yakinifu ikiwezekana mwaka wa fedha ujao tuanze ujenzi mara moja ili wananchi wa Mwanza na Kanda ya Ziwa na Tanzania kwa ujumla wanufaike na mpango wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wa kuhakikisha kwamba anaendeleza bandari hii kavu ya Fela.

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Maji; Mheshimiwa Pascal Lucas Lutandula.

Na. 36

**Hitaji la Maji Chato Kusini**

**MHE. SELINA H. KINGALAME K.n.y. MHE. PASCAL L. LUTANDULA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza zoezi la kutoa Maji Buzirayombo na kupeleka Chato Kusini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Pascal Lutandula, Mbunge wa Chato Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha inakamilisha utekelezaji wa miradi ya maji inayoendelea ili ianze kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi kabla ya kuanza ujenzi wa miradi mipya. Kwa sasa, Serikali inaendelea na utekelezaji wa jumla ya miradi mitatu (3) katika Wilaya Chato yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 41.3 ukiwemo mradi wa miji 28 wa Chato ambapo umefikia wastani wa 76% za utekelezaji na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Desemba, 2026.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa mradi wa miji 28 wa Chato kutaiwezesha Serikali kuanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa kutoa maji katika tanki lililopo Mlima Katende - Buzirayombo kwenda Kata zote tisa za Jimbo la Chato Kusini kwa gharama ya shilingi bilioni 22.1. Aidha, Serikali imeanza utekelezaji wa mpango wa kufikisha huduma ya maji kwenye vijiji 1,575 nchi nzima ambavyo havijafikiwa na huduma vikiwemo vijiji vitatu vya Butobela, Kakora na Mabila vilivyopo katika Jimbo la Chato Kusini.

**SPIKA:** Kwa niaba ya Mheshimiwa Lutandula.

**MHE. SELINA H. KINGALAME:** Mheshimiwa Spika, ninamkushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili.

Swali la kwanza, je, ni lini wananchi wa Nyakasiku Kata ya Buserere watapata maji ikiwa tanki la maji lipo kwenye maeneo yao na wao hawana maji?

Swali la pili, ni upi mpango wa Serikali kupeleka huduma ya maji safi katika Mji Mdogo wa Nyakayondwa wenye wakazi zaidi ya 70,000?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza na swali la pili ni dhamira ya Serikali kwanza kabisa kuendelea kumalizia miradi iliyopo. Pia, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaenda kukamilisha mradi wa vijiji 1,575 ambapo tumevigawa katika awamu tano na mwaka wa fedha 2026/2027 tunaanza na vijiji 314 na baadaye tutaendelea kufanya hivyo kwa kadri itakavyokuwa inawezekana.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha vijiji vyote vilivyobaki 1,575 viwe vimekamilika ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mamlaka ya hali ya hewa imetangaza kwamba mvua mwaka huu zitaanza mapema na kwa kuwa Halmashauri ya Mji wa Ifakara tuna mradi wa tuta la Mto Lumemo ambalo limepasuka kutokana na mvua za mwaka jana na Wizara ya Maji iliahidi kwamba itaziba eneo hilo haraka iwezekanavyo.

Je, ni lini Serikali itaziba Mto Lumemo ulipokatika ili kuzuia athari za mafuriko katika mvua zijazo kwa wananchi wa Jimbo la Kilombero?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na nimshukuru sana Mheshimiwa Asenga kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya, kubwa zaidi ni kuendelea kutupatia hali halisi ya mazingira yaliyopo katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji nipende kutoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa Bonde Wami-Ruvu

aende kuchukua hatua stahiki kwa sababu hili bwawa ni chanzo cha uhakika cha maji ambayo wananchi wanayategemea na sisi hatutoruhusu chanzo hiki kipate changamoto hiyo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, tunaenda kulichukua kwa uzito stahiki ili kuhakikisha kwamba wananchi wake wanaona kwamba maji yao hayapati changamoto na kuleta madhara katika mazingira yaliyozunguka pale.

**SPIKA:** Mheshimiwa Alan Thomas.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza niishukuru Serikali kwa kutupatia gari jipya *RUWASA* – Kakonko, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, tuna mradi wa maji wa Kabale ambao umekwama kwa zaidi ya miaka mitatu, kwa sababu tayari kwenye bajeti ya mwaka huu imewekwa, ni ipi kauli ya Serikali kuhakikisha mradi huo unajengwa ikiwa ni pamoja na ule wa Kihomoka wa kuchimba kisima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mvano kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba nipokee pongezi kwa niaba ya Serikali inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu yeye ndiye anayewezesha kuhakikisha kwamba watendaji wetu wanapata vitendea kazi na yeye amekuwa sauti ya wananchi wa Kakonko kuhakikisha kwamba watendaji wetu wanaweza kutekeleza majukumu yao kwa urahisi sana na ndiyo maana Mheshimiwa Rais alinunua vitendeakazi na Kakonko mmepata. Ninakupongeza pia kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na miradi ambayo inaendelea, tunayo miradi mingi na bahati nzuri Bunge lako Tukufu limetusaidia sana kupitisha sheria ya tozo ya mafuta. Fedha hizo sasa zinakuja moja kwa moja na tayari tumeshapokea

awamu ya kwanza ya fedha na tumeshaanza kuwalipa wakandarasi na tutaendelea kulipa awamu kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, lengo letu na maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha kwamba tunakamilisha miradi inayoendelea na miradi ambayo imekaa kwa muda mrefu kabla hatujaanza miradi mingine, nimtoe hofu mradi wake tunaenda kuupatia kipaumbele ili uweze kutekelezwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri amekuja Bunda ameona miradi ya takriban shilingi bilioni 14 imesimama ukiwepo na mradi wa kimkakati wa kutoka Migungani kwenda Mlima Kaswaka wa shilingi 1.7 *billion* kwa ajili ya kuondoa upotevu wa maji.

Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wananchi wa Bunda wanapata maji safi na salama ili dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan itimie?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Hata hivyo, nitumie fursa hii kumpongeza sana Dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya, ni kweli kabisa nimeshafika Bunda, lakini pia katika kuzingatia mahitaji ya Bunda na kwa kuangalia tathmini tuliyoifanya, tukaamua kufanya mabadiliko ya kiuongozi lengo likiwa kuleta tija katika utendaji ulioko pale.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Mheshimiwa Bulaya anafahamu kulikuwa na bomba ambalo takribani kilometa 4.1 ambalo lilikuwa linaleta changamoto ya upotevu wa maji kwa asilimia kubwa, hivi sasa Serikali ilichukua hatua kwamba hilo tunaelekea hatua za mwisho kabisa kulikamilisha ili lisiwe tatizo tena katika kupoteza maji ambayo ni uwekezaji mkubwa sana wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amekuwa sauti kubwa sana kwa Wanabunda, nimtoe hofu huu mradi ambao umebaki, Serikali tunaenda kuupa kipaumbele kuhakikisha kwamba unakamilika. Lengo la kwanza ni kuzuia upotevu wa maji ambao ni sawa na uwekezaji mwingine, lakini pia wananchi wake wataweza kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kumpongeza na sisi Wizara ya Maji chini ya Mheshimiwa Waziri Aweso tutakupa ushirikiano kuhakikisha kwamba changamoto zote zinatatuliwa ndani ya Jimbo lako la Bunda Mjini. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Amosy Maganga.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninakushukuru sana kunipa hii nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, huko Sikonge tuna bwawa letu la Ulua ambalo linahudumia Kata mbili, Kata ya Kiloleli pamoja na Kata ya Kipanga, bwawa hili ni la zamani na chujio lake limechakaa sana.

Je, ni lini sasa Serikali itatufungia chujio jipya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, chujio linapochakaa maana yake kwamba kuna madhara ya wananchi kupata maji ambayo si salama, ninaomba nipokee kwa niaba ya Serikali, tutatuma wataalam wetu kwenda kufanya tathmini ili tuone linahitaji nini, ili tuweze kupeleka fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunalirekebisha ili liweze kuendelea kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha. Sasa ni wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 14 wa Mheshimiwa Spika ambao ni wanachama wa Chama cha Ilala *Friends* kutoka Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Jaffar Kinega. *(Makofi)*

Wageni wengine watano wa Mheshimiwa Spika ni Kamati ya Siasa kutoka Wilaya ya Temeke Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wengine watano wa Mheshimiwa Spika ni Maafisa wa Benki ya *NMB* ambao wanaratibu Bunge Bonanza kwa ushirikiano na Ofisi ya Bunge, Ndugu Vicky Bishubo, Mkuu wa Huduma za Benki kwa Serikali. Ndugu Janeth Shango, Meneja wa Kanda. Ndugu Josephine Kulwa, Meneja Mwandamizi wa Mahusiano ya Benki na Serikali. Ndugu Grace Matemu, Meneja Mahusiano Mwandamizi wa Bunge na Ndugu Badiel Erasto. *(Makofi)*

Pia, wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wageni 50 wa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika Mstaafu na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU),* Kikundi cha *Capacity Buildings*. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 13 wa Mheshimiwa Dkt. Evaline Wilbard Munisi, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano, Kikundi cha *Love and Light* kutoka Wilaya ya Kinondoni Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi, Naibu Waziri Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Familia yake ya kutoka Jijini Dar es Salaam na Peramiho. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa John John Nchimbi, mwanafunzi wa Taasisi ya Uhasibu *(TIA)* Kampasi ya Mbeya Ndugu Tizostawa Lwena. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mwamengo Ulimboka Baraka, rafiki zake kutoka Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Wajumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Temeke Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando, viongozi kutoka *Zan Security* huyu ni 'Baba Levo' kwa jina lingine. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo, rafiki zake kutoka Mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Yahaya Esmail Nawanda hawa ni viongozi wa dini kutoka Wilaya ya Newala - Mkoani Mtwara. *(Makofi)*

Wageni 122 wa Mheshimiwa Mwantum Mzamilu Zodo, wanafunzi na walimu kutoka Shule ya Sekondari Rosmini ya Jijini Tanga. Pamoja na Mheshimiwa Zodo, wenyeji wao wengine ni Mheshimiwa Moses Sungura. *(Makofi)*

Wageni 73 wa Waheshimiwa Wabunge kutoka Wilaya ya Temeke, Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Temeke Jijini Dar es Salaam. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa maana ya ushangiliaji huu, furaha hii ni kama lile goli la Chama tu. *(Kicheko)*

Wageni 20 wa Mheshimiwa Mohamed Abdulla Makame, Kikundi cha Vijana wa Dijombi kutoka Mjini Magharibi Zanzibar. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Spika ambao ni Balozi Ali Jabir Mwadini, Katibu wa Rais. Brigedia Jenerali Nyamburi Mashauri, Mpambe wa Rais. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ni Brigedia Jenerali Nyamburi Mashauri, Mpambe wa Rais. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA YA KUTHIBITISHA UTEUZI WA MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu tarehe 25 Agosti, 2026 aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi, alijiuzulu wadhifa wake huo kwa mujibu wa Ibara ya 50(2)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, ili kujaza nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa Ibara ya 47(4)(c) ya Katiba, tarehe 26 Agosti, 2026 Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Taifa, ikiongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilimteua aliyekuwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Ibara ya 48(2) ya Katiba, Makamu wa Rais aliteuliwa kwa mujibu wa Ibara ya 50(4) ataapa kwa kushika madaraka yake baada ya uteuzi wake kuthibitishwa na Bunge. Uteuzi huo utathibitishwa na Bunge kwa kura za Wabunge walio wengi.

Waheshimiwa Wabunge, leo tarehe 28 Agosti, 2026 ndiyo siku maalum iliyopangwa kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais. Utaratibu wa zoezi zima utafafanuliwa na Katibu wa Bunge baada ya maelezo yangu. Hivyo, naomba Wabunge wote kuwa watulivu na kufuata maelekezo ili zoezi letu liweze kufanyika kwa haraka na ufanisi.

Waheshimiwa Wabunge, ninauthibitisho wa barua ambayo nimeipata asubuhi hii kutoka kwa Rais na ninamtaja rasmi, jina

lililoletwa ndani ya Bunge leo na kuchukua nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa barua hii iliyotoka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu toa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nitoe hoja ya kuliomba Bunge lako Tukufu lithibitishe uteuzi wa Mheshimiwa Deogratius John Pancras Ndejembi kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa Ibara ya 50(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kanuni ya 42 ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Bunge lako Tukufu limejulishwa, nafasi ya Makamu wa Rais iko wazi baada ya aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kupoteza sifa za kuwa Makamu wa Rais kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo na kwa kuwa kutekeleza masharti ya Ibara ya 50(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inataka Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amemteua Mheshimiwa Deogratius John Pancras Ndejembi, kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Uteuzi ambao kwa mujibu wa Katiba unapaswa kuthibitishwa na Bunge kwa kura za Wabunge walio wengi kama ambavyo umekwisha kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sifa za Makamu wa Rais zilizobainishwa katika Ibara ya 47(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Deogratius John Pancras Ndejembi anatosha. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, sina shaka Bunge lako Tukufu litakukbaliana na mimi kuwa kiti kimepata mtu sahihi wa

kumsaidia Mheshimiwa Rais majukumu kwa mujibu wa Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitaaluma, Mheshimiwa Deogratius John Pancras Ndejembi ana Shahada ya Uzamili katika masuala ya Usimamizi wa Biashara kutoka Chuo Kikuu cha *Cumbria* nchini Uingereza, Shahada katika masuala ya Uhusiano wa Kimataifa kutoka Chuo Kikuu cha *Lincoln* nchini Uingereza, na ana Stashahada ya Juu katika Usimamizi wa Utawala kutoka katika Taasisi ya Kimataifa ya Usimamizi wa Utawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafasi ya Makamu wa Rais ni nafasi yenye dhamana kubwa katika uongozi wa nchi yetu. Kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 47(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais ndiye Msaidizi Mkuu wa Rais kuhusu masuala yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla. Aidha, atamsaidia Rais kufuatilia utekelezaji wa siku hadi siku wa masuala ya Muungano, pia atafanya kazi zote atakazoagizwa na kutekeleza kazi za Rais wakati Rais hayuko kazini au yuko nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 47(8), Makamu wa Rais hutekeleza madaraka yake chini ya uongozi na usimamizi wa Rais na huwajibika kwake kuhusu mambo au shughuli atakazokabidhiwa na Rais.

Mheshimiwa Spika, majukumu hayo yanahitaji mtu mwenye uzoefu wa uongozi, uelewa mpana wa shughuli za Serikali, uwezo wa kufanya kazi kwa karibu na Rais na busara katika kushughulikia masuala ya kitaifa pamoja na uwezo wa kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Yohana 1:47: "Basi Yesu akamwona Nathanaeli anakuja, akanena habari zake, Mwisraeli kweli kweli, hamna hila ndani yake." Mheshimiwa Rais amemteua Mheshimiwa Deogratius John Pancras Ndejembi kwa kuzingatia, pamoja na mambo mengine, uzoefu alioujenga katika uongozi wa kisiasa na katika nafasi mbalimbali Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika Mheshimiwa Deogratius John Pancras Ndejembi, si mgeni katika uongozi wa umma na katika siasa za nchi yetu, amekuwa akijihusisha na shughuli za Chama Cha Mapinduzi kuanzia kwenye jumuiya kwa kipindi kirefu. Akiwa Mjumbe wa Baraza Kuu, amewahi kuwa miongoni mwa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi kupitia Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi, na mwaka 2020 alichaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Chamwino, nafasi iliyompa fursa ya kuwawakilisha wananchi na kushiriki moja kwa moja katika shughuli za Bunge na katika utekelezaji wa sera za Serikali. Aidha, kabla ya kuwa Mbunge, Mheshimiwa Ndejembi alihudumu kama Mkuu wa Wilaya katika Wilaya ya Kongwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchaguliwa kuwa Mbunge, Mheshimiwa Ndejembi ameendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kupewa majukumu mbalimbali ndani ya Serikali. Amehudumu kwa nafasi ya Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na amehudumu kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Kazi, Ajira pamoja na Vijana na Watu wenye Ulemavu. Amehudumu pia kama Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kwa sasa alikuwa Waziri wa Nishati.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi ambacho amehudumu ndani ya Serikali, Mheshimiwa Ndejembi ameonesha uwezo wa kubeba majukumu mbalimbali na kufanya kazi katika sekta zenye mahitaji na changamoto zinazotofautiana.

Mheshimiwa Spika, uzoefu huo ni muhimu kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais ambaye kwa nafasi yake atatakiwa kuwa tayari kumsaidia Mheshimiwa Rais katika masuala mbalimbali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutekeleza majukumu yote atakayoambiwa kwa mujibu wa Katiba na atakayoagizwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uteuzi huu pia unamleta mbele yetu kiongozi ambaye ana uzoefu wa kufanya kazi katika mihimili na

ngazi mbalimbali za uongozi wa umma na uzoefu wa uwakilishi wa wananchi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi yake kama Waziri wa Nishati, ni Mjumbe wa Baraza la Mawazi; na amekuwa Mjumbe wa Baraza la Mawaziri kwa zaidi ya miaka miwili mfululizo. Amefanya kazi katika Wizara na ofisi zenye majukumu mtambuka na ana uelewa wa masuala ya maendeleo na uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sifa na uzoefu huu, vinamwezesha kuwa msaada kwa Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu mazito ya kuiongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa msaidizi wa karibu wa Mheshimiwa Rais katika kutimiza majukumu yake. Kwa kuzingatia majukumu ya kikatiba ya Makamu wa Rais niliyoyaeleza, pamoja na uzoefu wa kisiasa, kiutawala na kiutendaji, Mheshimiwa Deogratius John Pancras Ndejembi, anatosha. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaamini kuwa ana uwezo wa kutekeleza kwa uaminifu na kwa ufanisi majukumu ya nafasi ya Makamu wa Rais na kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuendeleza shughuli za Serikali na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na wasifu huu katika utumishi, elimu aliyonayo pamoja na uzoefu, Mheshimiwa Deogratius John Pancras Ndejembi anao uzoefu mkubwa katika shughuli za Serikali, anatosha. Uzoefu huo unampa uelewa mpana wa mfumo wa Serikali na mahitaji ya wananchi katika maeneo mbalimbali ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo na kwa heshima na taadhima, ninaliomba Bunge lako Tukufu, kwa mujibu wa Ibara ya 50(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na kwa mujibu wa Kanuni ya 42 ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za Mwaka 2025, lithibitishe uteuzi uliofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Mheshimiwa Deogratius John Pancras Ndejembi kuwa Makamu

wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima na kwa unyenyekevu mkubwa, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, na hoja ikiungwa mkono lazima watu wachangie. Tuwape fursa baadhi ya Wabunge wachache kwa dakika tatu tatu au nne, mchangie hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na hatimaye tutaingia katika hatua zinazofuata kwa mujibu wa Kanuni na Katiba ya nchi yetu. Ninamwita sasa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi. *(Makofi)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi angalau na mimi niweze kutoa neno kwenye pendekezo na hoja ambayo imetolewa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninatoa shukurani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuongoza Taifa letu na kwa kuendelea kuwaamini Watanzania mbalimbali katika nafasi, na kwa kipekee, nafasi ambayo tunaitaja hapa ni pendekezo la Makamu wa Rais Mteule wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndugu yetu Mheshimiwa Deogratius John Pancras Ndejembi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu yetu Mheshimiwa Ndejembi, mimi ninamfahamu tangu alipokuwa Mkuu wa Wilaya ya Kongwa. Alipokuwa katika Wilaya ya Kongwa, kulikuwa na matatizo ya migogoro ya wafugaji na wakulima katika Wilaya ya Kiteto ambayo ipo Mkoa wa Manyara, lakini mara kwa mara matatizo yale yalikuwa yanaiathiri pia Wilaya ya Kongwa.

Mheshimiwa Spika, kwa umahiri mkubwa, maarifa makubwa na kwa umadhubuti wa kiuongozi, aliweza kushirikiana na viongozi wenzake katika Wilaya ya Kongwa kuhakikisha kwamba madhara yale hayakuleta athari katika Wilaya ya Kongwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, baadaye akashiriki katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na hatimaye wananchi wa Jimbo la Chamwino wakamwamini na kuwa Mbunge wao. Alivyokuja ndani ya Bunge, tumeendelea kuishi naye katika mazingira ambayo ameonesha umahiri mkubwa katika uongozi katika nafasi zote ambazo ameweza kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na ameonesha unyenyekevu, ucha Mungu, weledi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, nina imani kwamba Bunge hili Tukufu kwa heshima ya Rais na kwa imani ambayo Mheshimiwa Rais amempa Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, Waheshimiwa Wabunge tutakwenda kumthibitisha kwa 100% ya kura za ndiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, kwa mujibu wa maandiko, "mke mwema anatoka kwa Mungu", lakini mke bora kwa hapa Tanzania anatoka Tanga. Mimi Mheshimiwa Ndejembi ni mkwe wangu, ameoa Tanga. Wakati wanakuja kuomba maombi ya kuwapatia mke, wakati tunafungua ile barua na mimi kugundua kwamba huyu amelelewa vizuri kwa maadili ya Chama cha Mapinduzi akiwa katika nafasi ya Mjumbe wa Baraza la Umoja wa Vijana, basi nikawasihi wazee wenzangu kule nyumbani kwamba mtoto wetu atakuwa katika mikono salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, ninaomba Waheshimiwa Wabunge tuungane mkono kuhakikisha kwamba, kwanza tunampa Mheshimiwa Rais heshima kwa uteuzi huu ambao ameufanya, pia tunampa imani ya kushirikiana na mwenzetu huyu katika jukumu hili kubwa na zito ambalo Taifa linatarajia kutoka kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma, halafu jiandae Mheshimiwa Nollo.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu Makamu wa Rais Mteule.

Mheshimiwa Spika, kweli tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini tunakipongeza pia na Chama cha Mapinduzi kwa kuafiki na kukubaliana na pendekezo la Mheshimiwa Rais, kumpitisha Mheshimiwa Deogratius Ndejembi. Tumekuwa naye humu Bungeni. Kwanza, akiwa Naibu Waziri, Waziri kamili; Waziri amehama na mara ya mwisho anateuliwa, anatokea kwenye Kamati ya Nishati ambayo mimi ni Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninazungumza kwa niaba ya Kamati yangu ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Subira. Tuna furaha kubwa sana kumtoa Mheshimiwa Deogratius, lakini tuna masikitiko sana kumpoteza kwenye Kamati yetu, na tunamwomba Mheshimiwa Rais anapotuteulia Waziri mwingine, angalau afanane na Mheshimiwa Deogratius. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kusema neno moja. Nimeamini maneno yanayosema, ukifanya kazi kwa bidii, cheo kitakutafuta chenyewe.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mimi nilikuwa na Mheshimiwa Deogratius na baadhi ya Wajumbe wa Kamati, tulikuwa safarini kule Marekani. Wakati Mheshimiwa anapokea *message,* tulikuwa ubalozini pale, ndiyo anatutambulisha akiwa amekaa mbele. Hebu pata picha anayewatambulisha anaanza kudondosha machozi, halafu na nyie ni wageni. Tunajiuliza kimetokea nini? Baadaye akasema, nina mkutano mwingine. Ndiyo akaondoka hivyo. Kwa hiyo, kile cheo kimetokea akiwa haelewi, na hajawahi kumpiga *shoti* mtu humu. Wote ni marafiki. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, ungeruhusu watu wote wamzungumzie Mheshimiwa Deogratius, tungepiga kura saa 11.00. Hii inatupa

picha nzuri sana. Tunawapenda na tunawaamini sana viongozi wetu. Tuamini katika tulivyonavyo. Huwezi ukapata cheo kwa kumpiga *shoti* mwenzio.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amefanya pendekezo la busara kubwa sana, na hii inaonesha picha. Jiaminini kwenye kazi mlizopangiwa. Maana yake, kikubwa kinachowafuata nyuma, kitawafuata kwa bidii yenu na siyo kwa kupiga shoti watu wengine. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuwashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kama ni baraka ambayo tumepata kwenye Bunge letu hili ni kumtoa Mheshimiwa Deogratius. Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, nafasi aliyoaminiwa na Mheshimiwa Rais kwa umri wake, nimejaribu kuangalia viongozi waliokaa hicho kiti chake, yeye ndio namba moja kwa umri mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taifa hili tunakoelekea ni la vijana *Gen Z*. Sasa amepewa akafungue milango. Tunahitaji kupata viongozi vijana, wenye mawazo mepesi, wanaotumika na walio na nidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatutegemei kwa Mbunge mwenzetu ambaye ametoka humu, akaanze tena mambo yaliyotufikisha hapa. Sisi kama wenzake, tunamwomba kwa niaba ya Taifa hili na Bunge hili, aende akamsaidie Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia. Taifa tunamtegemea na tunamtegemea Mheshimiwa Mama Samia, hatuhitaji kumwona akiwa kwenye *stress* na uongozi. Tunahitaji kuona maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kwa haya machache, ninawaomba Wajumbe wenzangu, Waheshimiwa Wabunge, tupige kura kwa 100% kwa sababu huu ni uzao wetu na mimi inaniaminisha, kama ni *vetting* imefanyika. Kwa kweli Mungu awabariki sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nollo, Mheshimiwa Tauhida, jiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua Mheshimiwa Deogratius John Luis Pancras Mtemi Ndejembi, kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi ni mtoto wa John Luis Pancras Ndejembi na mama yake ni Amina Sharif ambao ni wakazi wa Moshi, Mtaa wa Mbuyuni. Mimi nimemfahamu Mheshimiwa Deogratius Ndejembi mwaka 1993, na mwaka 1994 nilivyomaliza darasa la saba, nikaenda kuishi kwa baba yangu mkubwa Mzee Pancras Ndejembi. Kwa hiyo, tumeishi nyumba moja; yeye akiwa darasa la sita na mimi nikiwa ndiyo nimemaliza darasa la saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, mimi katika ukoo ni ndugu yangu. Ukoo wetu ni mkubwa, unaitwa ukoo wa Wanyagundu, ni ukoo wa Kusila. Kwa hiyo, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi ni ndugu yangu wa damu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumefahamiana tangu enzi hizo, lakini kubwa, na niliseme hapa, mwaka 1995 mimi na ndugu yangu Mheshimiwa Deogratius Ndejembi tulikuwa katika mnada wa zamani wa Mailimbili. Tukasema sisi tupambane mpaka tuje kuwa viongozi. Hapo mimi nikiwa *form one*, yeye yuko darasa la saba na tukaweka kitu tukakiita *vision 1995*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mungu sikuwahi kuwaza kama *vision* ile itakuja kuwa pana kiasi hiki. Kwa hiyo, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi ni mjukuu wa Pancras Ndejembi ambaye amekuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma tangu mwaka 1982 mpaka 2007. Vilevile, Mzee Pancras Ndejembi aliwahi kuwa Mkuu wa Wilaya katika wilaya mbalimbali ikiwemo Moshi, Handeni na Ukerewe kule Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Ndejembi busara yake ni tangu akiwa mtoto na ninataka niseme, Mheshimiwa Rais ameweza kumpata mtu ambaye ana hekima kubwa katika umri

wake, lakini ni mtu mwenye upendo. Mheshimiwa Deogratius ni mtu mwenye upendo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na busara hii kubwa aliyonayo, amekuwa na uwezo na uhimilivu katika mawimbi mbalimbali ya siasa. Kwa hiyo, tumepata kiongozi ambaye mimi ninaamini atamshauri Mheshimiwa Rais na kumsaidia kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka niwaambie ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kiongozi ambaye Mheshimiwa Rais amemteua, kazi iliyofanyika ni kubwa, tumepata kiongozi safi ambaye ana moyo wa kutoa, na huwezi ukamtilia shaka hata chembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninawaomba wote tumpe kura zote za kutosha ili kuonesha heshima hii ambayo Mheshimiwa Rais ametuamini, Mbunge mwenzetu aliyetoka katika Bunge hili kupata nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, ahsante sana. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tauhida Gallos, Mheshimiwa Agnesta, jiandae.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuweza kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, nimepata kigugumizi cha kumzungumzia kaka yangu Mheshimiwa Deogratius. Nimepata kigugumizi kwa sababu nina mambo mengi ambayo ninamfahamu na kumjua. Natafuta pakuanzia lakini nitaenda pale kaka yangu alipopagusia kwenye suala la upendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, bado anatuona kama vijana lakini tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumpenda Rais wetu. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa

kutulindia Mheshimiwa Rais wetu na kumpa afya njema ili kuweza kulisaidia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kaka yangu Mheshimiwa Deogratius ana upendo mkubwa. Mungu ameendelea kuweka maono ndani ya Mheshimiwa Rais ili kujua nani na kwa wakati upi anaweza kumsaidia. Kaka yetu Mheshimiwa Deogratius ana upendo ambao mimi nikiendelea kuuelezea upendo alionao, ninaweza nikajisikia ninatoka machozi.

**SPIKA:** Sasa mengine usiseme, zungumza tu ya siasa. *(Kicheko)*

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, upendo wake kwa Taifa, au kwa wenzake pia ni mkubwa. Ninakumbuka wakati tuko Umoja wa Vijana, alikuwa anafanya kazi ya kutuhudumia. Kila anapokwenda safari masomoni, akirudi, jambo la kwanza alikuwa anahakikisha anakuwa na vijana wenzake karibu, kwa mfumo huo huo wa kukaa karibu, kuleta hata kile ambacho yeye anakipata huko anapokwenda, kuleta fikra mbadala wakati sisi tukiwa Wenyeviti wa Mikoa, na vilevile tukiwa Wajumbe wa Baraza Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deo, kaka yetu ambaye tunatarajia siyo muda mrefu tutampatia kura zote za Ndiyo, amekuwa ni mtu mwenye maono, amekuwa mtu mwenye kumtanguliza Mungu, amekuwa mtu mwenye kushika mikono wenzie, amekuwa mtu ambaye unaweza kumfikia kwa haraka. Kitu ambacho kwa sasa, baada ya muda mfupi, nina uhakika nitaki-*miss* ni lile neno "Dada Tahu", ninajua nitaki-*miss* kutoka kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hayo tu, ninaamini kuna Wabunge wengi vijana wanamfahamu vya kutosha. Tuna mambo mengi ambayo tungeweza kumwelezea, lakini kwenye hayo, wakati tunakwenda kumpa kura, tumpe neno dogo, "kafanye kazi ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, kafanye kazi ya kulisaidia Taifa hili, fanya kazi ya kuwashika mkono vijana wenzio, usituangushe.

Ukienda kufanya jambo lolote la kutuangusha, unawaangusha vijana wenzio."

Mheshimiwa Spika, tumepokea kile ambacho ametuletea Mheshimiwa Rais kwa upendo, kwa furaha, na tutahakikisha tunaendelea kuwa na Taifa hili na viongozi wetu. Tunachokisema, tunaomba Waheshimiwa Wabunge tumpe kura za Ndiyo ambazo zitaenda kumpa heshima Rais wetu, zitaenda kumpa nguvu na yeye za kwenda kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa fursa hii ya kuweza kuchangia. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Agnesta, atafuatiwa na Mheshimiwa Bashe, halafu Mheshimiwa Kingu ajiandae.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi asubuhi ya leo niweze kuchangia machache kuhusiana na hoja iliyo Mezani, hoja ya mteule wetu kwa maana ya kaka yangu Mheshimiwa Ndejembi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya kambi ya wachache walioko Bungeni, ninaomba nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo ameweza kumpendekeza kaka yetu Mheshimiwa Ndejembi ili aweze kwenda kumsaidia, na kuwa ni sehemu ya mafanikio katika uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kama Agnesta Lambert Kaiza, nitakwenda kumwongelea kaka yetu Mheshimiwa Ndejembi kwa vile ninavyomfahamu ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa undani kabisa nimemfahamu kaka yangu Mheshimiwa Ndejembi ndani ya Bunge hili Tukufu. Kwa uchache kabisa niseme, tumepata au tunakwenda kumpata Makamu wa Rais ambaye ana sifa na vigezo vyote vya kumsaidia Mheshimiwa Rais, na wananchi wote kwa maana ya Bara na Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ndejembi ni mtu ambaye tangu nimekuwepo katika Bunge hili la sasa na lililopita, ninamfahamu kwamba ni kiongozi mwenye upendo, ni kiongozi anayeunganisha zaidi badala ya kugawa. Hata mimi kama mpinzani, ninadiriki kusema kwamba Mheshimiwa Ndejembi hajawahi kabisa kuonesha utofauti hata wa masuala ya vyama vya siasa, zaidi sana amekuwa akituchukulia wote kwamba ni wa Taifa moja.

Mheshimiwa Spika, hivyo, ninamtakia kila la heri kaka yangu Mheshimiwa Ndejembi nikiamini kwamba ule upendo, mshikamano, kusaidiana sisi kwa sisi, hakutaisha kwa vile anakwenda kuwa Makamu wa Rais, lakini sasa atakwenda kuzidisha zaidi kwa sababu anakwenda kushika nafasi kubwa, nafasi ya namba mbili ndani ya hii nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa machache kabisa, ninaomba niseme, mimi mwenyewe nitakwenda kupiga kura ya Ndiyo kumthibitisha kaka yangu Mheshimiwa Ndejembi kuwa Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona, nimtakie kila la heri kaka yangu Mheshimiwa Ndejembi. Tutaendelea kumfanyia maombi ili aende kuwa baraka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ukikaa hapa, unamwona kila mtu; nani anafurahi, nani kachukia, nani ana huzuni? Nami ninawaandika wote wale ninaowaona. Leo cha ajabu, Mheshimiwa Sigrada Mligo kapiga makofi. Hii inaonesha chaguo hili ni chaguo la Mungu kweli. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Bashe, ajiandae Mheshimiwa Kingu.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia na kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kufika asubuhi ya leo. La pili, Mwenyezi Mungu hupitisha jamii kwenye nyakati mbalimbali kwa sababu maalumu na kwa malengo maalumu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008, baada ya Uchaguzi wa Baraza Kuu na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Vijana uliofanyika Dodoma, miongoni mwa Wajumbe wa Baraza Kuu walioteuliwa na Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni, kuwa Wajumbe wa Baraza Kuu, alikuwa ni Mheshimiwa Deo Ndejembi, Mheshimiwa Njalu, Mheshimiwa John Nchimbi, Mheshimiwa January Makamba, pamoja na mimi. Ndio tulioteuliwa na Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni kuwa Wajumbe wa Baraza Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengi wetu tunamfahamu Mheshimiwa Deo, na ninaamini kuwa jina la mzazi ndiyo limekwisha leo. Baada ya kura sasa siyo mzazi, atakuwa na mamlaka makubwa ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuwaamini vijana wanaotokana na Jumuiya ya Umoja wa Vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na historia ya mzee Ndejembi, lakini Mheshimiwa Deo ni zao la Chama Cha Mapinduzi. Ni mtu aliyetokana na CCM, na sio aliyepitia CCM. Kwa hiyo, anafahamu misingi ya chama hiki, anafahamu dhamana ya chama hiki iliyopewa, anafahamu wajibu wa chama hiki kwa Taifa hili, na anafahamu na amelelewa kwa misingi ya kuheshimu viongozi na walio juu yake.

Mheshimiwa Spika, tumeishi na Mheshimiwa Ndejembi, leo ni zaidi ya miaka 16 au 17. Mheshimiwa Deo ndiye Mjumbe mmojawapo kati ya wachache ndani ya Baraza Kuu; pande mbili zinapokuwa zinavutana, alikuwa na uwezo wa kukutana na pande zote na zote zikamsikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi letu, hatuna wasiwasi juu ya uwezo wake, hatuna wasiwasi juu ya tabia yake kama alivyosema Mheshimiwa Musukuma ya kutokupiga shoti wenzie. Hatuna mashaka juu ya nidhamu yake. Hatuna mashaka juu ya *exposure* yake. Ana historia ya *private sector*. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, nina jambo moja ambalo ninataka niliseme kwenye Bunge hili. Mwaka 2015, Mheshimiwa Deo aligombea Ubunge na kura zikapigwa. Ninataka niongelee suala la uvumilivu.

Mheshimiwa Spika, wakati akiwa na matokeo yake mkononi, akaja kunywa chai *Dodoma Hotel.* Yule pale ananisikia. Matokeo yaliyotangazwa Chamwino, siyo yale aliyokuwanayo mkononi, na Halmashauri Kuu na Kamati Kuu ya Chama ikamteua aliyetangazwa. Mheshimiwa Deo alikusanya mizigo, akasema, *Alhamdulillah*, ninarudi zangu, ninasubiri maelekezo. Akakaa akasubiri, akaja akapata u-*DC*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu humwandikia mtu kadari yake. Jambo moja la msingi, tumpe ushirikiano. Amepewa dhamana kwenye nyakati ngumu na tofauti na nyakati nyingine zozote katika nchi yetu. Anahitaji kupewa moyo, anahitaji kupewa *support*, na pia anahitaji kuombewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kura hizi tutakazompa leo, ambazo mimi sina mashaka, moja ni kumpelekea ujumbe Mheshimiwa Rais kwamba tumemkubalia ombi lake na kumhakikishia kwamba tutampa *support* msaidizi wake ili aweze kufanya naye kazi na kumpatia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ninataka niwaombe Watanzania, Taifa letu limetoka kwenye changamoto kubwa sana huko nyuma. Tuna Taifa moja. Tuunganeni sote kuwaunga mkono viongozi wetu ili tuweze kukabiliana na changamoto zinazokabili Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kila nyakati Taifa hupitia changamoto zake na kila nyakati Mwenyezi Mungu huwapatia viongozi wake.

Tuwape *support* viongozi wetu ili tukabiliane na changamoto za Taifa letu, tuweze kujenga Taifa moja. Hatuna Tanzania nyingine zaidi ya hii. Leo Tanzania hii Mwenyezi Mungu ameandika kwamba Rais ni Mheshimiwa Dkt. Samia, na Makamu wake ni Mheshimiwa Deo Ndejembi kuanzia baada ya kuapishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wabunge, na Bunge lako Tukufu, hatuna mashaka na Mheshimiwa Deo. Tumeishi naye mtaani akiwa *hustler*, akiwa raia wa kawaida, akiwa anajitafuta, akiwa kwenye kampuni za *telecom*, akiwa mtaani, akiwa Mjumbe wa Baraza, akiwa anatamani Ubunge wa Chamwino ambao ameukosa, amekuwa *DC*, amekuwa Naibu Waziri, amekuwa Waziri na leo kadari ya Mwenyezi Mungu imeandika awe Makamu wa Rais wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hatuna mashaka naye. Tuunganeni sote kulijenga Taifa hili. Tushirikiane, tusaidie viongozi wetu kurudisha umoja na mshikamano katika Taifa hili. Tunahitaji Taifa lililo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kingu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kutoka kwenye mizizi ya moyo wangu, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa neno katika kumwelezea Makamu wa Rais Mteule, kaka yangu Mheshimiwa Deogratius Ndejembi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninataka nilipe taarifa Bunge lako Tukufu, na Watanzania wanaotufuatilia katika jambo hili asubuhi ya leo. Neno la Mungu katika Kitabu cha Mithali 19:21 linasema; "Mnayo mipango mingi moyoni mwa mtu, lakini shauri la Bwana ndilo litakalosimama." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka nikuhakikishie, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amelipa Bunge lako heshima kubwa iliyotukuka. Kwanza Rais angeweza kumtoa Makamu wa Rais nje ya Bunge hili, na bado tungempitisha, lakini kitendo cha Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kumwamini Mbunge mwenzetu na kumteua kama Makamu wa Rais, linathibitishia Taifa letu *beyond reasonable doubt* kwamba Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni mama mnyenyekevu anayewapenda vijana wa Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uteuzi wa kaka yangu Mheshimiwa Deo Ndejembi, hauwezi kuachwa bila kutambua na kuthamini *commitment* kubwa Rais wetu aliyonayo na imani kubwa aliyonayo kwa vijana waliolelewa kwa malezi ya unyenyekevu, uadilifu, uzalendo, ucha Mungu na kulipenda Taifa kama alivyodhihirisha Rais kwa kaka yangu Mheshimiwa Deo Ndejembi siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwaambia Watanzania wanaotufuatilia na kutusikiliza kwamba Taifa letu kwa uteuzi alioufanya Rais, nchi yetu imepata kijana mwenye kaliba ya kuwapenda watu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taifa letu limepata kaliba ya vijana wanyenyekevu na wanaojishusha, vijana wakarimu na wapenda watu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiachilia mbali rekodi ya unyenyekevu, uzalendo na upendo wa Makamu wa Rais Mteule, ninataka Watanzania wajue Mheshimiwa Deo Ndejembi ni kijana mchapakazi mwenye *commitment* ya uzalendo kwa nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dunia ilipokuwa inapita kwenye misukosuko ya gharama za mafuta kupanda, ni kijana huyu Mheshimiwa Deo Ndejembi alisimamia Serikali kuhakikisha Shirika letu la *TPDC* linapata uhakika wa kupata mafuta katika Taifa kwa kipindi chote ambacho dunia inapita katika misukosuko mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwa uzalendo huo wa kijana huyu ameweza hata kuling'arisha Taifa kwa uwezo wake wa kuliwakilisha Taifa hata katika medani za kimataifa. Mheshimiwa Deo anapokuwa nje ya nchi, mnaona uwakilishi wake na utulivu wake namna anavyoliwakilisha Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitamke neno hili, na wakati mwingine nikiwaambia watu humu kuwa mimi ni mtumishi wa Mungu, wengine wanafanya masihara. Ninataka nikwambie, miezi miwili iliyopita, Mungu alizungumza na mimi, na nilimpigia simu Mheshimiwa Deo, na nilimtumia *message* Mheshimiwa Deo Ndejembi; yuko hapa. Nilimwambia kuna jambo Mungu anakwenda kukufanyia, nimefunuliwa na Mungu, yuko shahidi, atatoa ushahidi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilimtumia ujumbe, na Mheshimiwa Deo kama ninasema uongo atathibitisha. Nilimtumia ujumbe wa kwamba Mungu amezungumza na mimi nimekuona unapanda kwenye *red carpet*. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninataka nikuthibitishie, uteuzi wa Mheshimiwa Deo Ndejembi, kwa sababu mimi ni mpakwa mafuta wa Bwana, umetoka kwa Bwana mwenyewe. Aende akamtumikie Mungu. Nafasi aliyopewa kaka, Mheshimiwa Deo imetoka kwenye mboni ya jicho la Mungu mwenyewe. Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia ametumiwa tu na Mungu kum-*endorse* yeye kuwa msaidizi wake.

Mheshimiwa Spika, neno langu la mwisho kwa kaka yangu Mheshimiwa Deo Ndejembi, kama alivyosema kaka yangu Mheshimiwa Hussein Bashe, Taifa letu limepita kwenye misukosuko mingi. Rais wetu ameonesha utulivu mkubwa kuhakikisha Taifa letu linaendelea kuwa moja. Mama huyu amepigwa mishale mingi, ameendelea kutulia na kuhakikisha anasimamia Katiba na kuwatunza Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rai yangu moja kwa Mheshimiwa Deo, aende akamfanye Rais wetu apate utulivu. Aende akamfanye Rais wetu awe na matumaini makubwa ya kutekeleza ahadi

tulizozitoa kwenye kitabu cha Ilani ya kuwatumikia Watanzania na kuwaletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanasubiri barabara, maji, umeme, na miundombinu. Mheshimiwa Deo aende akamsaidie Rais, na sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tunampa ahadi moja kwamba tutakuwa wanyenyekevu kwake, kwa Rais na kwa Waziri Mkuu, na tutakuwa wanyenyekevu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninataka nikwambie, ninarudia tena, nilisema hapa, Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia kwa mapenzi na kwa ulinzi wa Mungu wetu wa Mbinguni atamaliza kipindi chake salama, atalivusha Taifa letu salama, na sisi Watanzania tutaendelea kumwombea Rais wetu na kumtia moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mungu ambariki Rais wetu, Mungu alibariki Taifa letu. Mungu aongeze uzalendo kwa Watanzania, tulipende Taifa letu, kwani hatuna mama mwingine zaidi ya mama Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Mungu ambariki kaka yangu Mheshimiwa Deo Ndejembi, neema ya Mungu iendelee kuwa naye, wapigwa magoti na wapakwa mafuta wa Mungu tutaendelea kumlilia Mungu katika uso wake, amtunze na kuimarisha Serikali yetu kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuna orodha ndefu kidogo na muda unakwenda na Mheshimiwa Deogratius ana majukumu, akitoka hapa tu anaanza majukumu. Kwa hiyo, hawa wengine niwaombe tupunguze muda kidogo ili tuweze kuendelea kwenye zoezi lenyewe ili tuweze kukamilisha ili aende kwenye majukumu mengine.

Sasa ninamwita Mheshimiwa Ali King, atafuatiwa na Mheshimiwa Mavunde, ajiandae Mheshimiwa Shabiby na Mwenyekiti wa Dodoma, Mheshimiwa Simbachawene, atafuata Mheshimiwa Profesa Kabudi, Mheshimiwa Doto na tutamalizia na *Attorney General.*

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai katika siku ya leo kuja kushuhudia haya ambayo yatafanyika hapa leo. Maana ya makamu ambavyo imeelezwa kwenye Katiba yetu ni msaidizi, lakini maana ya makamu, ukitazama katika kamusi, ni mtu wa makamo. Maana mtu wa makamo ni kutoka miaka 35 mpaka miaka 60. Kwa hiyo, ndugu yangu Mheshimiwa Deogratius, kwa mujibu wa sifa zake zilizoelezwa hapa, pia kwa mujibu wa tafsiri ya makamu, huyu ni mtu sahihi katika hii nafasi ambayo yupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna sifa nyingi sana zimetajwa, lakini mimi nimefanya naye kazi wakati yupo katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu. Pale palikuwa pana taasisi hizi ambazo ni mifuko ya hifadhi. Sote sisi ni mashahidi, sasa hivi mifuko ya hifadhi inafanya kazi vizuri kwa sababu ilipitia katika mikono yake. Tulibadilisha sheria tofauti, tulitengeneza vitu tofauti tofauti, leo wanaweza wakaingia mpaka wamachinga katika mifuko ya hifadhi, ni kwa sababu ya jitihada zake hizo tuliziona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme neno lingine ambalo ni muhimu sana, katika nafasi ya Makamu, maana yake ni msaidizi kama ilivyoelezwa hapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa sifa yake Mheshimiwa Deogratius, msikivu, mnyenyekevu, hajikwezi, ni mtu mwenye maono. Hii ndiyo sifa na tabia zake zilivyo kwa maana hiyo inaendana na hiki cheo cha Makamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamwamini Mheshimiwa Deogratius kwa jambo moja. Yeye atakuwa msaidizi. Mheshimiwa Deogratius anao uwezo na lkulu, anapajua pa kwenda kumshauri Mheshimiwa Rais. Kwa hili, tunamwelewa sote. Pia, tunamwelewa Mheshimiwa Deogratius kwamba ana uwezo wa kuchapa kazi katika majukumu ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema kitu kimoja, wakati yuko katika Wizara ya Ardhi, alikuwa ameanzisha mambo mengi sana pale, ambapo mpaka sasa hivi yanaendelezwa kwa ajili ya kuwasikiliza watu kwenye migogoro ya ardhi. Mimi mwenyewe ni shahidi na

anafanyia kazi papo kwa hapo, na wala huwezi kumpelekea kesi ya uongo labda kwa sababu wewe ni Mbunge ukapata haki. Huwezi kupata haki kama huna haki. Atafuatilia na atalifanyia kazi kwa wakati ule ule na utapata jawabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tumeletewa jina sahihi, lenye umri sahihi, katika wakati sahihi na sisi tunachohitajika tufanye, ni maamuzi sahihi. Maamuzi sahihi ni kuthibitisha jina lake kwa kupiga kura ya Ndiyo kwa 100% ili kazi zetu na nchi yetu iende mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inapita katika kipindi ambacho ni kizuri sana. Tunaweza tukasema ni kizuri, siyo kibaya. Tunapopata mtu mzuri wa kumshauri Mheshimiwa Rais, tutakwenda vizuri zaidi. Kwa hiyo, ili twende vizuri zaidi, Bunge hili lifanye mazuri leo ya kuthibitisha jina kwa 100%. Ninakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mavunde, wajiandae Mheshimiwa Shabiby na Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa nafasi hii. Kwanza kabisa, ninamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uteuzi wa Mheshimiwa Deogratius John Pancras Ndejembi, Makamu wa Rais Mteule, ikiwa ni nafasi ya karibu kabisa ya usaidizi kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya miaka 43 iliyopita Mkoa wa Dodoma katika viunga vya mitaa ya Uzunguni, Kata ya Mbabala Chizomoche na Kata ya Kikuyu, anasimama kijana wa Kitanzania, kwa majina ya Deogratius John Pancras Ndejembi. Ameishi maisha ya kawaida ambayo wameishi Watanzania wengi sana. Ameishi katika mazingira ambayo ingawa yalikuwa ni mazingira ya mjini lakini kwa muda mrefu alijielekeza zaidi katika maisha kama yale ambayo watu wengi waliyaishi vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo iliyopo hivi sasa Mamlaka ya Maji pale *DUWASA* ndiyo eneo lilikuwa la mwisho. Baada ya pale,

ulikuwepo msitu mkubwa sana kwenda mpaka katika ukumbi wa Jakaya Kikwete. Eneo lile lilijawa na wanyama mbalimbali wakiwemo digidigi. Miaka hiyo ya tisini, tukiwa na umri wa miaka tisa na nane, mimi nikiwa na miaka nane, Mheshimiwa Deogratius akiwa na miaka tisa, tulikuwa tunaongoza kundi la vijana wenzetu kwenda kutega mitego ya kukamata digidigi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara zote tulikuwa tunaongozwa na mbwa ambao walikuwepo pale katika eneo la Uzunguni; mbwa wakali, na mmoja alikuwa akifahamika kwa jina la *Fox*. Tulikuwa tukienda nao katika msitu ule, lakini digidigi aliyekuwa akipatikana kwa umri wetu tulikuwa tunagawana wote nyama, na kurudi nyumbani, kila mtu na safari yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1992, Kanisa la Mtakatifu Paul wa Msalaba, Jimbo Kuu la Dodoma, lilitupokea mimi na Mheshimiwa Deogratius Ndejembi tukiwa wasaidizi wa altare *(altar boys)* chini ya Askofu Marehemu Mathias Isuja na Msaidizi wa Paroko, Marehemu Askofu wa Jimbo la Kondoa, Bernadin Mfumbusa. Tukaenda Mafundisho ya Kipaimara na Komunio, wote pamoja, pale katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Paul wa Msalaba.

Mheshimiwa Spika, nimepata nafasi ya kumfahamu Mheshimiwa Deogratius Ndejembi kabla hajawa na nafasi, mtu mwenye upendo, mwenye kujali watu na ambaye mara zote aliwatanguliza wenzake mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vijana wa Dodoma tuliokuwa hapa, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi ndiye alikuwa kijana wa kwanza kuwa na uwezo wa kuendesha trekta, Massey Ferguson la Mzee Ndejembi. Ilikuwa trekta lile likimaliza kilimo, alikuwa anatoka nalo kwa kificho kutoka kwa babu yake, Mzee Ndejembi, anakuja kutupitia mitaani tunatembea nalo kwenye trekta, yeye akituendesha. Ninamfahamu kama mtu rahimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012, akiwa anatoka masomoni Uingereza, pale Dar es Salaam, ipo nyumba iliyokuwa ikimilikiwa na mzee wake, baba yake, Mzee John Luis Pancras Ndejembi, lakini Mheshimiwa Makamu wa Rais Mteule ali-*opt* kuja kukaa

pamoja na mimi Mtaa wa Akachube, Kijitonyama, ambapo tumeishi naye kwa pamoja na akaiacha nyumba yake pale Kamata na tukaanza harakati za kisiasa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nikiwa Mwenyekiti wa Vijana wa Mkoa wa Dodoma, aliniambia anatamani sana kufanya siasa ya UVCCM. Wakati huo, ndani ya UVCCM kulikuwa kuna mvutano mkubwa sana, makundi mawili yanavutana. Nikamwambia Makamu wa Rais Mteule, ndugu yangu Mheshimiwa Deogratius, ninajua wewe ni rafiki yangu, lakini huku nilipo mimi usije, nenda sehemu nyingine, lakini tubaki tunaheshimiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida, hii ilimfanya mwaka 2008 wakati ule akapata uteuzi wa kuwa Mjumbe na tukaendelea kuheshimiana, wote tukiwa tunavutana ndani ya UVCCM. Upande wake yeye mwingine, na sisi mwingine. Pia, wote tukapata bahati ya kupitishwa kugombea nafasi ya Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM kupitia kundi la vijana.

Mheshimiwa Spika, katika uchaguzi ule, tukachaguliwa wote kwa pamoja, na yeye ndiyo alitembea Tanzania nzima kutuombea kura. Mimi pamoja na Mheshimiwa Jerry Silaa, tukateuliwa kuwa Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM kuwakilisha vijana. Tumeishi pamoja ndani ya UVCCM akiwa kiongozi mwenye mapenzi makubwa sana na watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadaye wote tukafikiria kwenda kugombea Ubunge, na siku ya kuchukua fomu, tulikwenda pamoja kuchukua fomu ya Ubunge, wakati Ofisi za Wilaya ya Chamwino zikiwa pale Ofisi ya Dodoma, tuliongozana kwa pamoja. Mwenyezi Mungu akajalia mchakato ukaenda kama alivyosema Mheshimiwa Bashe, na pale nilimheshimu sana ndugu yangu Mheshimiwa Deogratius Ndejembi. Alikuwa na matokeo yake kama alivyosema, kikatokea kilichotokea, lakini akanipigia simu kwamba, ndugu yangu, mimi sijafanikiwa, ninakutakia kila la heri, Mungu akuongoze, madhali wewe umekuwa Mbunge, mimi nina amani kubwa sana. Ngoja mimi nikaangalie maisha mengine. Huyu ndio Mheshimiwa Deogratius Ndejembi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, leo ninasimama hapa kwa furaha kubwa sana juu ya maisha ya Mheshimiwa Deogratius Ndejembi na kazi nzuri ya siasa aliyoifanya mpaka leo kumfikisha hapa.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, ndugu zangu, ninataka niwahakikishieni kwamba Mheshimiwa Deogratius Ndejembi hajawahi kubadilika, amebaki kuwa yule yule katika maisha yake yote. Tumpe imani, tumpigie kura za kutosha ili leo Mheshimiwa Rais aamini kabisa kwamba chaguo alilofanya ni sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, Walatini wana msemo wanasema *Vox populi, vox Dei,* yaani sauti ya wengi, ni sauti ya Mwenyezi Mungu. Leo Bunge hili limethibitisha, kwa wingi wetu, ni sauti ya Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Shabiby, atafuatiwa na Mheshimiwa Simbachawene, halafu Mheshimiwa Profesa Kabudi, Mheshimiwa Biteko na Mwanasheria Mkuu wajiandae.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mmoja wa wachangiaji. Kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Rais, kwa fumbo. Fumbo alilotuwekea hapa, sisi tulikuwa tuna-*point* wazee, wazee tu. Mzee fulani, mzee fulani, sasa baadaye tukaja kuona katokea *Gen-Z*.

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi nilivyoona kwenye mtandao, nikajua hizi habari ni feki. Nikampigia Mheshimiwa Lusinde, nikamwambia Mheshimiwa Lusinde ni kweli au ni mitandao? Mheshimiwa Lusinde akaniambia, kweli mjomba. Nikamwambia basi nimeamini sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba, Mheshimiwa Deogratius ninamfahamu kwa muda mrefu, toka akiwa mdogo. Ninamfahamu sana sana; siyo ninamfahamu kidogo. Mheshimiwa

Deogratius alikuwa ni kama mdogo wangu, rafiki wa mdogo wangu mkubwa, na saa nyingine alikuwa anakuja Gairo, anakaa hata mwezi mzima tuko naye pale. Akitoka pale, anakwenda kwenye mambo yake mengi mengi.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa Mavunde, alikuwa anapenda sana kuendesha matrekta, na pale kwetu palikuwa na matrekta. Kwa hiyo, alikuwa anagonga gonga, mara kagonga hiki mara kagonga hiki. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamfahamu toka akiwa mdogo, ni muda mrefu. Hata wakati anakwenda kugombea Ubunge, sisi ndio tulikuwa washauri wake. Ninakumbuka nilimpa mipira, nikamwambia wewe nenda kagawegawe tu, huyo Mbunge aliyeko hapo ataanza kukutukana, kwa hiyo, atakuwa anakutangaza, wewe nenda tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninataka kusema, mimi nimesimama kwanza kuweka sawa. Kuna baadhi ya watu hata hawaelewi Mheshimiwa Deogratius ni kabila gani? Mheshimiwa Deogratius ni Mgogo. Kwa hiyo, watu wanapoandika kwamba Mheshimiwa Deogratius katokea upande fulani, upande fulani, Mheshimiwa Deogratius ni Mgogo. Mama yake naye ni mtu wa Kilimanjaro, lakini yeye ni Mgogo.

Mheshimiwa Spika, ninamfahamu Mheshimiwa Deogratius kuanzia kwa babu yake. Babu yake Mzee Ndejembi alikuwa Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Dodoma, lakini siyo Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Dodoma tu, alikuwa Mwenyekiti wa Wenyeviti wote wa mikoa, Tanzania Bara. Alikuwa Mwenyekiti wa wenyeviti wote wa mikoa wa Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cheo hiki ni kizuri sana, lakini nataka niseme tu na wengine ambao mko huko mbele, lazima mheshimu mtu aliyeshika mpini. Aliyeshika mpini, kashika mpini. Huwezi ukashindana na mtu aliyeshika mpini. Ndugu zangu tunawatakia mambo mazuri wote huko. Wewe ndugu yetu ambaye umeteuliwa kuwa Makamu wa Rais, tunajua kwamba uende

ukamsaidie Mama vizuri, Mama afanye kazi bila presha. Mlioko nao, nafasi za Urais bado, subirini kwanza ili mama afanye kazi kwa nafasi. Ndiyo ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukisimama watu kama sisi, lazima tunyooke kwenye ukweli. Twendeni tukamsaidie Mama, afanye kazi yake kwa nafasi. Asifanye kazi huku anasikia la huyu, huku anasikia la yule, huku majungu haya, na sisi Wabunge, kupigana shoti kama alivyosema Mheshimiwa Musukuma, tuache. Tusiwachanganye hawa watu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deogratius akawe kiunganishi kikubwa kati ya wananchi na Serikali kwa kumsaidia Mama. Hivyo atakumbukwa na kila mtu. Msiende kule, tuna kazi ya kujadili. Maana yake, kuna kipindi watu wanakaa hata Bungeni hapa, labda Mawaziri na Mheshimiwa Spika huna taarifa, lakini sisi tukikaa kule tunajadili habari ya Urais. Fulani atakuwa, fulani atakuwa, na ndiyo maana hata mimi wakati ule nikasema, na mimi nipo, msiniache, kwa sababu nimeona kama Urais ndio kila mtu anautaka, hata mimi nipo, na nina naibu wangu hapa, lakini sasa ninaona, basi cheo kimeshakwisha. Kwa hiyo, ninawashukuru sana, ahsanteni sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Haya Waheshimiwa, mmesikia mihimili hiyo na Bunge kuna mhimili hapa. Mmesikia kuheshimu mihimili? Basi, nafikiri mmenielewa. Mheshimiwa Simbachawene.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, mimi nimesimama kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kumpitisha mpendekezwa kwa nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie ndugu yangu na kwa leo kwa mara ya mwisho kabla hajawa Makamu, ninataka nimwite mdogo wangu, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi. Baada ya hapa ninajua sitapata kibali hicho tena. Yeye ni bosi, na mkubwa wetu, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa uongozi Mheshimiwa Deogratius ni mkubwa, ana uwezo mkubwa na ana uzoefu mkubwa. Alianzia kwenye nafasi za chama, Umoja wa Vijana, Ukuu wa Wilaya, Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imemchukua miaka sita tu alipoingia humu Bungeni kupitia nafasi ya juu. Hii ni neema na ni ibada kwake yeye. Aisali ibada hii kwa kutambua kwamba ni Mungu ndiye amemfikisha hapa. Pia atambue kwamba Mungu huyo amemtumia Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kufanya awekwe katika nafasi hii ambayo nimemwona tangu tunampokea asubuhi kwenye ndege pale, bado haaminiamini, bado haelewielewi. Sasa aelewe kwamba yeye ndiye anayekwenda kuwa Mheshimiwa Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deogratius amepatikana katika wakati sahihi, na mazingira sahihi. Yeye ni kiongozi wa kizazi kipya, na Mheshimiwa Rais ametumika na Mungu kuwapa suluhisho la tatizo la wakati, mazingira na aina ya kiongozi anayetakiwa. Yeye ni aina ya kiongozi anayetakiwa kwa sababu umri wake unaakisi huko mbele kwamba ndio vijana wanaotakiwa kulitumikia Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anakuwa Makamu wa Rais wa 13, Makamu wa Rais mwenye umri mdogo kuliko wengine wote waliopita tangu tupate uhuru. Udogo wake ni wa umri, lakini siyo udogo wa uwezo wa uongozi. Ninamfahamu, na rafiki yake mkubwa Mheshimiwa Mavunde amemzungumzia, mimi hawa ni wadogo zangu. Ninaposimama hapa, ninajivunia, na hata wakati mwingine ninapandwa na furaha kiasi cha kupitiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninajiuliza Mheshimiwa Deogratius yule aliyekuja kwangu akiwa haelewi hata kama Ubunge ataupata, ndio huyu leo ni Mheshimiwa Makamu wa Rais! Sitaki nifike kule mbali, lakini aniruhusu niseme hili tu, kwamba yule aliyekuwa hana hata fedha ya mafuta ya kutia kwenye gari kumalizia kampeni, akafika kwangu, akanitafuta mitaa ya Kaloleni halafu tukakutana,

nikamwambia mdogo wangu nilichonacho hiki mdogo wangu, nenda Mungu atakujalia. Leo anaenda kuwa Makamu wa Rais, Mungu ni mkubwa, Mungu ni wa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila mja na kila mtu ana kilele chake katika mafanikio. Unaweza ukaanza kufikiria ndiyo umeanza, kumbe kilele chako ndiyo kimefika, na mwingine anaeanza kumbe kilele chake kipo juu yake. Tumpende huyu kijana na tumsaidie.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ametupa zawadi sisi Wabunge, angeweza kumtoa Makamu wa Rais nje ya Bunge hili. Lazima tumwonyeshe imani aliyotupa Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha kwamba tunampa kura zote za Ndiyo Makamu wa Rais mtarajiwa, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka niseme, mimi ninabaki na furaha yangu moyoni, na niseme, na nijumlishe, pengine siwezi kujua Mungu amenipangaje, maisha yangu yanaishia lini, lakini yeye Mheshimiwa Deogratius Ndejembi na Mheshimiwa Antony Mavunde ambaye wakati anamaliza *Form Six,* baba yake alinikabidhi yeye.

Mheshimiwa Spika, leo ninasimama hapa, yeye ni Mheshimiwa Waziri. Alinikabidhi akiwa amemaliza *Form Six,* akanitafuta kule Vingunguti, tukala wote ugali wa mchana, leo wamekaa pamoja hapa, mwingine Makamu wa Rais na mwingine ni Waziri. Hongereni wadogo zangu, hongereni sana wanangu.

Mheshimiwa Spika, nitaendelea kuwapa *support* na kwa sasa tutam-*support* sana Mheshimiwa Deogratius ili asituangushe sisi wa Mkoa wa Dodoma, na mimi niliyemsimama hapa kuongea kwa niaba ya Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Dodoma, kama Mwenyekiti wao, na pia kwa niaba ya Watanzania wa Mkoa wa Dodoma...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mwenyekiti.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja, na tumpe kura zote za Ndiyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Kabudi, jiandae Mheshimiwa Doto Biteko, na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue fursa hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi nami kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kumthibitisha, mimi leo ninamwita kwa mara ya mwisho, mwanangu Mheshimiwa Deogratius kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu Rahimu wakiisoma Zaburi ya 136:1-4 "*Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema, kwa maana fadhili zake ni za milele. Yeye peke yake afanya maajabu makuu.*" Hakika, leo Mungu wetu, kwa kupitia mja wake mwema, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amemwona kijana, Mheshimiwa Deogratius John Pancras Mtemi Ndejembi, kushika nafasi hii ya Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uteuzi wa Mheshimiwa Rais, ambao hatuna budi kumshukuru, ni uteuzi mwanana kwa sababu nyakati hizi zinastahiki vijana wa aina ya Mheshimiwa Deogratius, na Deogratius maana yake ni "mshukuruni Mungu." Majina hubeba watu.

Mheshimiwa Spika, baba yake ni John. John, maana yake, ambalo pia ndilo jina langu, ni "*waliopendelewa na Mungu.*" Yeye amshukuru Mungu na amezaliwa na waliopendelewa, na Mungu atunze hilo katika maisha yake yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametuletea mtu sahihi kwa wakati. Mheshimiwa Deogratius John Lui Pancras Mtemi Ndejembi anazo sifa zote za kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile anazo sifa za ziada za kufaa kuwa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maana ya kuwa msaidizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninarudia, kwa mara ya mwisho kulitumia neno hili, "mwanangu Mheshimiwa Deogratius, tunza tabia ambayo umekuwa nayo maisha yako yote kabla Mungu hajakupa nafasi hii. Endelea kushika haya yafuatayo ambayo ninaomba niyaseme kwako. Ukiwa msaidizi wa Mheshimiwa Rais, ninakuomba uendelee kuwa na utii usiotiliwa mashaka; uendelee kuwa mwadilifu na mwaminifu, uendelee kuwa mtu mwenye heshima na staha kwa mkubwa wako kama ilivyo tabia yako; endelea kuridhika na kutunza ulichopewa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kawaida yake, na alizingatie, aendelee kuheshimu na kuzingatia kimo chake. Yeye anakwenda kuwa msaidizi wa Mheshimiwa Rais. Nimwambie, "mwanangu Mheshimiwa Deogratius zingatia hilo. Ila endelea na tabia yako ambayo umekuwa nayo siku zote, ya uvumilivu, kila mtu ameisema hapa ya uvumilivu; uvumilivu ambao wakati mwingine watu walidhani wewe ni dhaifu, kumbe ndiyo ilikuwa nguvu yako. Endelea kuwa mnyenyekevu ambapo watu wengine wakati mwingine walidhani hujui chochote, leo sifa zako zimesomwa na zimesemwa."

Mheshimiwa Spika, nimwambie Mheshimiwa Deogratius, aendelee kuwa mzalendo, aitumikie nchi yake kwa moyo wake wote, amsaidie Mheshimiwa Rais kwa moyo wake wote na kwa nguvu zake zote. Leo wengi wamesema kwamba amepata bahati kubwa ya kulelewa na babu yake ambaye tunamfahamu sisi, Mzee Pancras Mtemi Ndejembi kutoka Kijiji cha Chizomoche labda niseme leo, huko ndipo anapotoka Mheshimiwa Chinyele.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Chinyele na Mheshimiwa Deogratius ni watu wa kijiji kimoja. Baba yake ni rika za baba zetu, walimu kutoka upande huo ambao wamefanya kazi kwa uaminifu akiwa mwalimu katika shule za Kanisa Katoliki na baadaye katika shule za Serikali na baadaye katika uongozi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, zaidi malezi mazuri aliyoyapata kutoka kwa bibi yake, Mdala Lea Kasiani Pemanjee, mtoto wa Katekista Kasiani Pemanjee wa kutoka Nkhome, ndiye aliyemvuvia roho ya upendo, roho ya huruma, roho ya staha, na roho ya heshima. Nina hakika leo Mdala Lea yu hai, na leo amempa furaha kubwa. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan leo amemwongezea mama yetu Mdala Lea Kasiani Pemanjee miaka ya baraka kubwa kuuona ukuu wa Mungu katika nyakati hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi, ninayo furaha kubwa sana na moyo wangu umejaa furaha na shangwe kwa uteuzi wake; na sasa *privilege* yangu inakwisha. Jana wenzake wananiambia, kila siku alikuwa anapita hapa anakwambia, "mzee wangu ulimswanu? Nami ng'untya mwanangu Deo nilimswanu."

Mheshimiwa Spika, leo imekwisha, yeye sio mwanangu tena. Kwa maana ya nafasi yake, yeye sasa ni Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwenye kimo kikubwa kuliko change. Mimi kwake sasa kimo changu ni kidogo, ni Waziri katika Serikali ninayotumika kwa ridhaa ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, kuanzia leo, ile lugha yangu ya zamani, "mwanangu tushirikiane," imekwisha. Sasa nipo tayari kupokea maelekezo na maagizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi na mke wangu Dkt. Amina Mheshimiwa Deogratius tulikuwa tunamwita mwenetu. Ajabu ya Mungu, mimi jina langu la ubatizo ni John, na baba yake ni John; mimi mke wangu ni Amina, na mama yake ni Amina. Kwa hiyo, kwetu alikuwa ni mtoto.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, leo yeye sasa ni Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania. Kwa mila zetu, mtoto anapopata ngazi hiyo, anaanza kuwa baba yako, siyo kwa maana ya kukuzaa, lakini baba yako kwa sababu amekuheshimisha. Ahsante sana kwa kuniheshimisha *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, baada ya jambo hili, na Mheshimiwa Keneth Nollo yupo hapa, wazee wamenitumia ujumbe nimsomee, na nitausoma ujumbe huo halafu nitamaliza kwa aya ya Biblia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niusome ujumbe huo ambao Mheshimiwa Nollo ni shahidi kwa lugha waliyonitumia; "*Ikonje limaga mwi konje - Anye Wanyangudu mli watemi wagona, Kukuyo ali mtemi Pancras, Kusila alimtemi ne wakukuzo wose wa Nollo Kusila wali watemi. Alu agwe Deo si uli Mtemi. Wawa ikutu lya Mtemi. Wawa mutazi wa Mtemi. Taze mahweso maswanu Mtemi we Si yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Mtima wako Wose. Mulungu yakulugute. Mulungu yakudime na Mulungu yakupele nk'ojo zose lawa zuwali sunga miaka ne chibitilila.*"

Mheshimiwa Spika, wanasema, "tawi la mti bora hutoka katika mti bora. Ninyi ni wanyangundu, mna asili ya watemi waaminifu. Babu yako Mzee Pacras alikuwa mtemi, Kusila alikuwa mtemi na babu zako wote; Nollo, Kusila walikuwa watemi, lakini wewe leo siyo mtemi, bali ni sikio la mtemi. Wewe leo ni msaidizi wa mtemi. Mpe mawazo mazuri na ushauri mzuri Mtemi wa nchi yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa moyo wako wote. Mungu akubariki, Mungu akulinde na akujaze baraka zake zote."

Mheshimiwa Spika, maana haya yanatoka kwa wazee wake wote wa Bihawana, wa Bahi, wa Chikuyu, wa Maweni, wa Sorya, kose, kose, kose. Hapa Manyoni yote, Bahi yote, Dodoma Vijijini yote, wazee wamenipa ujumbe huu nimsomee. Sasa, nimalize na maneno kutoka Waraka wa Kwanza wa Mtume Paulo kwa Timotheo 4:12. "Mtu yeyote asikudharau kwa kuwa wewe ni kijana, bali uwe kielelezo kizuri kwa waumini katika usemi, mwenendo, upendo, imani na usafi." Nenda, kama walivyosema wote, tunza nafasi uliyopewa, msaidie Mheshimiwa Rais ili aweze

kuliongoza Taifa hili kama ambavyo Mwenyezi Mungu amempangia aliongoze.

Mheshimiwa Spika, mpe amani, mpe utulivu wa akili, lakini kama nilivyosema wakati mmoja, ayashikilie sana maneno ya mwadhama Polycarp Kadinali Pengo wakati wa kuwekwa wakfu Askofu Elinaza Sendoro wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania Dayosisi ya Mashariki na Pwani, maneno aliyomwambia Msaidizi wa Askofu, wao wanamwita *Dean*, akasema, "mara nyingi msaidizi hukosea anapoona kila wakati mkubwa anampa mambo makubwa ayatatue. Asipokuwa na saburi, asipokuwa na hekima, asipokuwa na unyenyekevu, atadhani yeye ni sawa na mkubwa wake. Shika hilo, wewe ni msaidizi wa Mheshimiwa Rais."

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deogratius ana sifa zote, ana haiba hiyo, ana tabia hiyo na wenzake wote wa rika yake wameshuhudia. Sisi tulio wazee, furaha yetu ni kuwaona vijana watakaoliongoza Taifa hili baada ya sisi zamu yetu kuwa imekwisha, tuwatazame. Ndiyo maana tunaona fahari katika uzee wetu kuwa pamoja na ninyi vijana na hasa vijana wenye heshima, vijana wenye adabu, vijana wenye kiasi, vijana wenye kujua ukomo wao, vilevile vijana wanaothamini Taifa lao, wanaoipenda nchi yao na wanaoheshimu viongozi wao.

Mheshimiwa Spika na ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge wote, Ado, Ado!

*(Hapa Mhe. Ado S. Ado Alisimama)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU:** Mimi siyo mwalimu wako, lakini pia sisemi hivi kwa nia mbaya, la hasha, hili ni jambo la Kitaifa. Hili siyo jambo la vyama, ni jambo la Kitaifa."

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote, niwaambieni ndugu zangu, hakuna Taifa lingine tulilonalo, kama alivyosema msemaji mmoja hapa, isipokuwa Tanzania. Yote haya ni tisa, kumi ni uimara, usalama, amani, umoja, na mshikamano

wa Taifa hili la Tanzania, na hasa katika kipindi hiki cha tufani, misukosuko, ubarakala, na mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, hiki ndicho kipindi cha sisi Watanzania kujua tukiivuruga hii Tanzania hatuna kwenda kwingine. Haya yanakuja kwa sababu ya kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tu tumekwenda kushuhudia kuzinduliwa kwa Bwawa la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Lile siyo bwawa, lile ni ziwa. *That is a man-made lake* na ni la pili kwa ukubwa Barani Afrika na ndipo nilipomwona Mheshimiwa Deo amevaa nguo ya unyenyekevu kabisa. Hakuvaa suti, amevaa shati lile lile walilovaa watumishi wa *TANESCO*, lile lile. Sasa nikwambie mwanangu Deo kwa mara ya mwisho huo ulikuwa ndiyo mtihani wako na ukaufaulu kwa kuonyesha unyenyekevu wa hali ya juu siku ile na leo tuko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi Waheshimiwa Wabunge wote tutoe kura za ndiyo kwa 100%. Hizo zitambariki Mheshimiwa Deogratius John Pancras Ndejembi, zitampa nguvu lakini pia zitampa amani kubwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba tumemheshimu na tumethamini chaguo sahihi alilotuletea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaunga mkono hoja, ninaunga mkono hoja, ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko.

**MHE. DKT. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ameitoa mbele yetu muda si mrefu.

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba kwanza maneno aliyozungumza mtangulizi wangu Mheshimiwa Profesa Kabudi, mwanadamu yeyote ambaye anajua kusikiliza ni maneno

ambayo yanaweza kum-*move* kila mmoja na hasa yule tunayemzungumzia hii leo. Ninapata tabu sana kuyaharibu maneno yale kwa sababu moja; yanausia ndani yake, lakini kwa mara ya kwanza Wagogo wamepata bahati ya lugha yao kusemwa Bungeni tena kupitia Waraka wa Wazee wa Kigogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kuharibu maneno hayo ya Mheshimiwa Profesa Kabudi, Waziri wetu ninaomba nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye yeye hupanga majira na nyakati katika maisha ya wanadamu. Tunamshukuru Mungu sana, kwanza kwa zawadi ya uzima na afya, lakini kwa kufanya tukio hili litokee tukiwa hai, tukiwa tunaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ninamshukuru sana na kama walivyosema wenzangu, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kumwona kijana mwenzetu ndani ya Bunge hili ambaye wengi tumefanya naye kazi akaona kuwa inafaa amteue yeye kuwa msaidizi wake wa karibu. Kwa maana hiyo ametuheshimisha sana Wabunge, amewaheshimisha sana vijana na kubwa zaidi Chama Cha Mapinduzi ambacho kimempendekeza kumleta hapa kwenye ukumbi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaki kutoa siri za vikao, lakini ninataka kutoa ushuhuda mdogo. Shangwe ninayoiona hapa baada ya jina la mwenzetu, ndugu yetu Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi ilikuwa hivyo kama Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa niliyekuwa kwenye kikao baada ya Mheshimiwa Rais kuleta lile jina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chama Cha Mapinduzi, Halmashauri Kuu yake baada ya jina hili kutajwa hakuna hata mmoja aliyekaa, wote walisimama wakampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu ametuletea mtu sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwanadamu kwa asili hujulikana kwa namna tatu. Ajijuavyo yeye, Mungu anavyomjua na namna ambavyo wengine wanamjua. Hapa tunazungumzia namna

moja ambavyo wanadamu wengine wanavyomjua Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi. Wote hapo wamezungumza na hasara ya kuzungumza mwishoni ni kwamba utarudia waliyosema wenzio, lakini faida ni kwamba unaweza ukafanya uchambuzi wa yale waliyosema wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo ambayo ninapata faida kama mzungumzaji wa mwishoni mwishoni ni kwamba yapo mambo ambayo wote wanafanana katika kuyasema, wanamzungumzia Deo kama mtu msikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukikaa na Mheshimiwa Deo Ndejembi ukazungumza naye unaweza ukajiona una akili sana. Ana uwezo wa kukusikiliza hata kama anatofautiana na wewe. Mheshimiwa Deo ni mtu ambaye anakusikiliza ili akuelewe si sawa na wengine wanaokusikiliza ili wajiandae kukujibu. Yeye atakupa muda, atakusikiliza, hata kama hakubaliani na wewe, Deo atakwambia nimekuelewa. Mheshimiwa Rais tunamshukuru sana ametuletea mtu sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, lingine ambalo wote tunafanana katika kuzungumza kuanzia msemaji wa kwanza, mtoa hoja na baadaye Mheshimiwa Profesa Kabudi, tunakubaliana bila kumpamba kwamba Mheshimiwa Deo ni mtu mnyenyekevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, koti la unyenyekevu kama si lako hata ukilazimishwa kuvalishwa watu watasema; sawa lakini mh! Huyu? Humu wote wanakiri Mheshimiwa Deo Ndejembi ni mtu mnyenyekevu, anayekuwa rafiki wa kila mtu na hayuko hivyo tu Bungeni, yuko hivyo kila mahali. Nimepata bahati ya kufanya kazi naye akiwa Waziri wa Ardhi, si mtu ambaye anapenda kusema, anapenda kutenda zaidi. Mheshimiwa Deo angependa matendo yake yale yamzungumze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati fulani tulikuwa na kazi fulani tumetumwa, nikamwomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi tumeandikiwa *message* ya mama analalamika Dar es Salaam juu ya kero ya kudhulumiwa ardhi yake. Nikamwita Makamu wa Rais

mteule huyu nikamwambia hili jambo liko kwenye sekta yako twende ukatusaidie. Akaniambia nimelichukua, hakurudi hata kwangu kuniambia, hakurudi hata kwenda kwenye *media* kutangaza. Niliona yule mama anarudi anakuja kunishukuru mimi, nikamwambia yupo aliyefanya hiyo kazi. Akasema nimemtafuta kijana mpole yule amenisaidia jambo hili ambalo nimehangaika nalo kwa muda wa miaka mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yanayosemwa ndani wapo maelfu na mamia ya Watanzania wangepata nafasi tuliyonayo humu ndani, wangeyarudia kwa namna ile ile.

Mheshimiwa Spika, ninataka nikuhakikishie kwamba tumepata kiongozi ambaye moja ya kazi kubwa anajua kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Kabudi, anajua kumheshimu aliye juu yake, anajua kuheshimu anaofanya kazi nao na anajua kuheshimu wale ambao wanamsaidia kazi.

Mheshimiwa Spika, ninataka nimwombe Mheshimiwa Deo na sipo hapa kwa ajili ya kumpa wosia. Mara zote huwa tunaitana mwenecho kama wengine wanavyomwita majina mbalimbali, ninataka nimhakikishie kuwa hilo jina linakufa kuanzia leo. Yeye ni kiongozi wetu, Makamu wa Rais wetu, lakini muhimu zaidi msaidizi wa pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kazi yake kubwa ni kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la maana ambalo bahati aliyonayo anaenda kumsaidia mtu ambaye kwanza ana utu, anajali na anasikiliza. Wale ambao tumewahi kufanya kazi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tutakuwa mashuhuda hapa duniani na mbinguni. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hakunyimi nafasi ya kutumia ubongo wako kufikiri kubuni mambo mapya. Atakupa hiyo nafasi wakati wote kwa sababu tu yana maslahi kwa nchi. Aende akamsaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Waheshimiwa Wabunge pamoja na kura tutakazozitoa hapa ndani niwaombe jambo lingine ambalo sikulisikia kwa wengi wakilisema. Tuna dini zetu, hatuna cha

kufanya kwa ndugu yetu huyu; wacha tumwombee. Mungu amuimarishe. Kazi hii si kazi rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majaribu aliyokuwa anayapata akiwa Waziri yanapanda kiwango hata hayo majaribu yanakuwa ya *level* ya Makamu wa Rais. Mambo atakayokuwa anasikia atasikia mambo makubwa zaidi. Wataibuka watu kundi dogo la watu wanaoitwa wavunja moyo, kazi yao ni kuhakikisha kwamba hufanyi kazi yako unawafikiria wao. Hakuna namna atakavyosimama zaidi ya sala zetu. Tunamwombea kwa Mungu na sisi pamoja na wengine waliozungumza na ambao hawakupata nafasi ya kuzungumza, tutamwombea, tutamuunga mkono na tunamtakia kila la kheri kwenye majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimalizie jambo moja dogo. Mheshimiwa Deo alinialika jimboni kwake nikawa mgeni rasmi wakati anasoma utekelezaji wa Ilani mwaka mmoja uliopita. Ninataka nichukue nafasi hii niwapongeze sana Wanachamwino, niwapongeze sana wazazi wake, niwapongeze sana walimu wake, niwapongeze sana wale waliokuwa naye kazini, wale waliokuwa Mawaziri wake akiwa Naibu Waziri, wale waliokuwa wasaidizi wake kwenye ofisi zao walilea mtu ambaye kila mzazi hapa nchini angetamani kuwa na mtoto wa namna ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wanachamwino wakati nimekwenda kwao kwenye mkutano ule, jambo ambalo mimi mwenyewe nimekuwa Mbunge kwa muda sasa niliona Mheshimiwa Deo anatuzidi wengi. Alikuwa na uwezo katikati ya mkutano akakaa pembeni kuanza kusikiliza wananchi. Mimi nilimwambia Mheshimiwa katika utaratibu wako ulionao wa kusikiliza wananchi bila kuchoka, bila shaka Mungu ana kitu cha ziada ndani yako na leo kimethibitika kwamba Mungu ameamua yeye awe Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwaombe Wanachamwino wamwombee mtoto wao, ninajua watatakiwa kutafuta Mbunge mwingine. Watafute Mbunge wa aina ya Mheshimiwa Deo ili

aendelee kuwaunganisha Wanachamwino wabaki kuwa kitu kimoja.

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge humu ndani ya Bunge tutam-*miss* lakini tutamwombea. Moja ambalo ninamhakikishia awe na uhakika nalo ni kwamba kila Mbunge aliyemo humu tukiwemo sisi Wabunge ambao anatuacha leo, furaha yetu ni kumwona anafanikiwa, furaha yetu ni kumwona ana afya njema, furaha yetu ni kumwona anamsaidia Mheshimiwa Rais ili nchi hii iweze kwenda mbele kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashawishi na kuwaomba na kwa kweli mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza vizuri, Mheshimiwa Deo anatosha. Hilo neno tu anatosha lilitosha kumwelezea. Tutoe kura zetu zote isitokee hata moja itakayoharibika ili tupeleke salamu duniani kwamba chaguo la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa nafasi ya Makamu wa Rais ni chaguo sahihi, tunaliunga mkono na tuko tayari kushirikiana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa *Attorney General*, Mheshimiwa Hamza Said Johari.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu hoja ya kuuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake na kumteua Mheshimiwa Deogratius John Louis Pancras Ntemi Ndejembi kuwa Makamu wa Rais mteule ambaye baada ya kuthibitishwa na Bunge hili na baada ya kuapishwa na Jaji Mkuu kwa mujibu wa Katiba ashike madaraka ya Makamu wa Rais. Tunamshukuru sana kwa maono yake haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ndejembi ninamfahamu nimefanya naye kazi kama Mwanasheria Mkuu katika miradi mikubwa mikubwa mbalimbali ya Taifa hili. Ni mtu mwenye uwezo mkubwa, mwenye weledi, nidhamu na utiifu, lakini nikitaja watu ambao ninawafahamu wenye upendo na huruma, Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi ni miongoni mwa watu wenye upendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia aliyekuwa Makamu wa Rais kuwasilisha taarifa ya kujiuzulu na baadaye kupoteza uanachama wa chama cha siasa zimeibuliwa hoja mbalimbali za kikatiba kuhusu wakati ambao kiti cha Makamu wa Rais kinakuwa wazi na utaratibu unaopaswa kutumika kujaza nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali nina wajibu wa kutoa ufafanuzi wa kisheria. Kwa kuwa hoja hizo zinagusa Katiba ni vizuri tukaliweka jambo hili sawa kwa sababu kwenye mitandao ya kijamii kumekuwa na upotoshaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza; kwamba kiti cha Makamu wa Rais kiko wazi lini kufuatia barua ya aliyekuwa Makamu wa Rais aliyoiandika ikiweka tarehe rasmi *(effective date)* ni tarehe 4 Septemba na Mheshimiwa Rais amekubali. Kwa hiyo, kwa hali hiyo tarehe rasmi itakuwa tarehe 4 Septemba kwa mujibu wa Ibara ya 149(2).

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Ibara ya 149(2) inatambua kwamba mtu aliyetoa taarifa ya kujiuzulu basi tarehe ya kujiuzulu itakuwa ni ile siku taarifa hiyo imepokelewa au tarehe nyingine ya baadaye iliyotajwa kwenye barua hiyo. Kwa hiyo, hiyo ndiyo *scenario*. Maana yake ni kwamba ataendelea kuwepo madarakani mpaka tarehe 4 Septemba 2026.

Mheshimiwa Spika, sasa tunakuja kusema kwamba kwa kuwa maisha yanaendelea je, ni zuio yanapotokea mambo mengine ya kikatiba yanayomfanya apoteze sifa kwamba tunaendelea kusubiri tarehe hiyo? Ndiyo ufafanuzi ninaotaka kuutoa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 50(4) ambayo wengi ndiyo wamejikita kule, kwanza cha msingi kuelewa ni ibara inayoweka utaratibu wa namna ya kujaza nafasi hiyo. Sasa kwa kuwa ibara hiyo ya 50(4) na nitaisoma kwa sababu lazima tuelewe ikitokea kwamba kiti cha Makamu wa Rais kipo wazi kutokana na masharti yaliyomo katika ibara ndogo ya (3). Ibara ndogo ya (3) imejikita katika Bunge kumwondoa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, ibara ndogo ya (3); kifo au kujiuzulu basi mapema iwezekanavyo na kwa vyovyote vile ndani ya siku zisizozidi 14 baada ya kushika madaraka yake, Rais atamteua mtu atakayekuwa Makamu wa Rais na uteuzi huo utathibitishwa na Bunge kwa kura za Wabunge walio wengi. Kwa hiyo wengi walijielekeza kwenye ibara hii kwa kuwa suala la kuvuliwa uanachama halijatajwa hapa, basi kiti hakiko wazi.

Mheshimiwa Spika, sisi wanasheria kuna kitu kinaitwa *principles of statutory and constitutional interpretation* (ile misingi ya kutafsiri sheria). Moja ya misingi pamoja na misingi mingine ni msingi unaitwa *the doctrine of harmonious construction*, kwamba, unapokuwa unatafsiri vifungu vya Katiba na ukakutana na kifungu kinakutatiza ukiviangalia vingine, basi unatakiwa ufanye "*Harmonious interpretation*."

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu *issue* ni Makamu wa Rais, unataka kumjua huyo Makamu wa Rais ni nani na ana sifa gani? Kwa hiyo, unaachana na ibara hii, inabidi uende ukamfahamu. Sifa za Makamu wa Rais ni nani; maana hizo ndiyo sifa za Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, inasema Ibara ya 47(4) "Mtu hatateuliwa kugombea au kushika" maana nilimsikia mpotoshaji mmoja anasema ibara hiyo inahusu wakati wa kugombea tu, aah! Inasema "kugombea au kushika". Aliyekuwa Makamu wa Rais aligombea, Mheshimiwa Deogratius Pancras Ndejembi yeye anakuja kushika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo basi, mtu hatateuliwa kugombea au kushika Kiti cha Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano isipokuwa tu;

(i) Raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa Sheria ya Uraia. Kwani hiko kipo kule, si tumetaja tu Ibara ya tatu kifo au kujiuzulu? Kwa hiyo, kwa sababu hakijaandikwa kule, akichukua uraia wa kigeni tunakuwa na Makamu wa Rais kutoka nje? Haiwezekani! Tunatafsiri vipi vifungu wanasheria? Ndiyo! Akishachukua uraia wa kigeni tayari siyo Raia wa Tanzania, tayari hiyo sifa ameshaipoteza;

(ii) Ametimiza umri wa miaka 40;

(iii) Ni mwanachama na mgombea aliyependekezwa na Chama cha Siasa;

(iv) Anazo sifa za kumwezesha kuwa Mbunge au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi; na

(v) Katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi hajawahi kutiwa hatiani katika Mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba, upo uwezekano katika kipindi hicho kuelekea tarehe nne yatatokea mengine ambayo yakasababisha Kiti hicho kuwa wazi kabla ya tarehe hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiti kinakuwa wazi kwenye mazingira gani? Hilo nalo ni muhimu sana tukalielewa. Kinakuwa wazi katika mazingira yafuatayo:-

(i) Muda wake utakapokwisha, muda wa Makamu wa Rais ukiisha Kiti kiko wazi;

(ii) Akifariki dunia akiwa katika madaraka, likitokea hilo Kiti kitakuwa wazi tu;

(iii) Kujiuzulu;

(iv) Atakapoapishwa kuwa Rais baada ya Kiti cha Rais kuwa wazi na hili limetokea. Kwani hili limeandikwa kule, si wamesema kifo, kujiuzulu na masharti ya ibara ya kuondolewa. Kwa hiyo likitokea hili na hili lilitokea kwamba aliyekuwa Makamu wa Rais baada ya kifo cha Mheshimiwa Rais ameapishwa, hicho kiti kimeshakuwa wazi;

(v) Atakapotiwa hatiani kwa kosa la jinai linaloonyesha utovu wake wa uaminifu;

(vi) Atakapoapishwa Rais mwingine kushika nafasi ya Rais pamoja na Makamu wake;

(vii) Atakapoondolewa madarakani baada ya kushtakiwa Bungeni kwa mujibu wa masharti ya Ibara ndogo ya (3) ya ibara hii. Sasa hii ya mwisho mnisikilize vizuri;

(viii) Atakapoacha kushika Kiti cha Makamu wa Rais vinginevyo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

Mheshimiwa Spika, hutakiwi kuwa unaandika Katiba unajaza vitu unaweka moja inachukua mengine yote. Kwani si unaweza ukatokea ugonjwa aidha wa kimwili au wa kiakili, hawezi tena kwa sababu huku masharti ya Katiba, Makamu wa Rais ndiyo atakayemsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake, sasa hawezi anaumwa. Ndiyo hii (h) lakini (h) ndiyo inaenda kuyabeba yale yote, zile sifa zote. Kwamba amesita kuwa Raia wa Tanzania labda ameondolewa uanachama na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hii (h) atakapoacha kushika Kiti cha Makamu wa Rais vinginevyo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, likitokea hilo, hicho Kiti kiwazi. Sasa kiwazi lini? Siku ya

tarehe 26 Agosti, 2026, taarifa imekuja kwamba aliyekuwa Makamu wa Rais amevuliwa uanachama. Kwa hiyo, akivuliwa uanachama, huyu Makamu wa Rais ni nani, nimewatafsiria, hiyo sifa mojawapo hapo imeondolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa nilivyokuwa namsikiliza huyu wakili mmoja, yeye alisema kwamba sifa hizi ni kwa ajili tu ya kugombea. Kwa hiyo, huyu anayekuja kushika hazimhusu yaani kwa tafsiri yake yeye anataka kusema kwamba Mheshimiwa Rais wakati anateua mtu wa kuja kushika asizingatie hizi. Kwa sababu hizi ndiyo sifa hakuna Ibara nyingine iliyoweka sifa. Kwa hiyo, asipozingatia hizi, maana yake ni kwamba tutakuja kuwa na Makamu wa Rais ana miaka 25, *below 40*, au tunakuja kuwa na Rais kutoka nje ya nchi, ana Uraia wa Canada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi tunatafsiri vipi? Nimewashangaa sana wale mawakili, wanatafsiri vipi vifungu vya sheria? Yaani nchi hii iwe na Makamu wa Rais kutoka Sweden. Ndiyo maana tunasema Ibara ya 50(4) na hii ya 47 lazima ziwe-*harmoniously construed and interpreted* vinginevyo unaweza ukapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kitu kimoja cha msingi maana hii Ibara si wanasema kwa sababu haijataja kuvuliwa uanachama, kwa maana hiyo hii Ibara ya 50(4), Bunge ambalo linataka kufanya hii kazi leo, inatoa tafsiri tofauti. Je, tumeshawahi kuitumia ibara hii kwa jambo au mazingira yoyote ambayo hayajatajwa? Maana tumesema kifo, kujiuzulu na yale masharti ya Ibara ya tatu ambayo ni Bunge linapokuwa limemwondoa, je, tumeshawahi?

Mheshimiwa Spika, tumeona kule kwamba moja ya masharti ambayo yatasababisha Kiti cha Rais kuwa wazi ni atakapoapishwa kuwa Rais baada ya kiti cha Rais kuwa wazi. Kwa hiyo, Ibara ile haijataja imesema tu masharti ya Ibara ya tatu ambayo ni Bunge kumwondoa au kifo au kujiuzulu. Sasa huyu Makamu ameapishwa amekuwa Rais. Kwa hiyo, kwa kuwa haijatajwa hapa hicho kiti hakijawa wazi? Ndiyo tafsiri wanayojaribu kuiweka, haiwezekani *what kind of statutory interpretation is this? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, siku ya Jumanne tarehe 30 Machi, 2021, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alileta jina la Mheshimiwa Philip Isdor Mpango ndani ya Bunge hili kwa mujibu wa Ibara hii hii wanayoijadili na haijaandikwa hapa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema Ibara hii inaweka utaratibu yaani Bunge litamthibitishaje? Kwa hiyo, alithibitishwa siku ya Jumanne ya tarehe 30 Machi, 2021 na kesho yake siku ya tarehe 31 Jaji Mkuu wa nchi hii alimwapisha. Ndiyo maana sisi tumeona kwamba somo hili la *statutory interpretation* ambalo tunalisoma kule kwenye *legal method* tulitoe kule tulisome mwaka mzima. Kwa sababu ya changamoto hii, ninaona tunahitaji kulipa muda zaidi ili tutafsiri vifungu vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunatakiwa tupate muda zaidi kwa sababu hii inapelekea hiyo athari kwamba utatafsiri kifungu na kupelekea kwenye *absurdity*, kwa sababu kama unatafsiri kifungu kwenye mazingira hayo, tunaweza kuwa kwenye mazingira hayo mengine, hatutakiwi tu-*create* kiroja wakati unatafsiri ila tafsiri ilete *logic* na mantiki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, msingi wa kuwepo kwa hatua ya kuthibitishwa na Bunge hili ni kwa mujibu wa Ibara ya 47(2) na Ibara ya 48(1). Katika mazingira ya kawaida Makamu wa Rais anachaguliwa pamoja na Rais katika Uchaguzi Mkuu na anaingia madarakani pamoja na Rais hakuna shida. Katika mazingira hayo tayari anakuwa amepata ridhaa ya wananchi kupitia uchaguzi, lakini nafasi inapokuwa wazi katika kipindi mtu anayeteuliwa hajachaguliwa moja kwa moja na wananchi, ndiyo maana Katiba imeweka uthibitisho wa Bunge hili kwa wawakilishi wa wananchi wote ili ridhaa iwe imetolewa na Bunge kwa niaba yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi ni kwamba, taarifa ya kujiuzulu ingeweza kusababisha nafasi ya Makamu wa Rais kuwa wazi kuanzia tarehe 4 Septemba, 2026, lakini kabla ya tarehe hiyo kufika limetokea suala la kupoteza uanachama na limesababisha kupoteza sifa ya kushika Kiti kwa mujibu wa Ibara ya 47(4)(c) ya Katiba, ikisomwa pamoja na Ibara ya 50(2)(h) ile inayosema "litakapotokea jambo lingine lolote kwa mujibu wa Katiba".

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hakuna changamoto yoyote ya kikatiba na kama Serikali tutaendelea kuhakikisha kwamba tunazingatia Katiba katika maamuzi mbalimbali ambayo tunayafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja iliyowasilishwa na Waziri Mkuu kwamba tumthibitishe wote kwa pamoja Mheshimiwa Deogratius John Louis Pancras Mtemi Ndejembi ili baadaye aweze kuwa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana *AG* kwa *VAR*, imetupa elimu kubwa sana na sasa tunaendelea.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha utaratibu wa uchaguzi. Kama inavyoonekana kwenye Orodha ya Shughuli za Leo siku ya Ijumaa tarehe 28 Agosti, 2026, Bunge lina shughuli ya kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais kwa mujibu wa Ibara ya 48(2) na 50(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais umefafanuliwa na Kanuni ya 42 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, kama ifuatavyo:-

(i) Spika ataliarifu Bunge kuhusu uteuzi wa Makamu wa Rais na kutaja jina la Mbunge au mtu anayependekezwa na Rais kuthibitishwa na Bunge kuwa Makamu wa Rais, hatua ambayo imeshafanyika kwa Spika kumtaja Mheshimiwa Deogratius John Pancras Ndejembi.

(ii) Baada ya Spika kutaja jina la Makamu wa Rais anayependekezwa atamwita Waziri Mkuu ili atoe hoja ya kuliomba Bunge lithibitishe uteuzi huo. Jambo hili

limeshafanyika na Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatoa hoja hiyo.

(iii) Baada ya hapo kwa idadi ambayo ataona inafaa Spika ataruhusu Wabunge kuchangia hoja ambayo imeshatolewa na Waziri Mkuu na jambo hili limefanyika ambapo Wabunge 13 walipata fursa ya kuchangia hoja.

(iv) Zoezi la kupiga kura litaanza ambapo kila Mbunge atapewa karatasi moja kupiga kura moja ya NDIYO au HAPANA katika kisanduku husika.

(v) Spika atateua wawakilishi watakaosimamia na kuhesabu kura.

(vi) Baada ya zoezi la kuhesabu kura kukamilika Katibu wa Bunge atatangaza matokeo ya kura.

(vii) Mwisho Bunge litathibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais kwa kuzingatia asilimia ya kura za Wabunge walio wengi kwa mujibu wa Ibara ya 50(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa ninaomba zoezi la kupiga kura kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais lianze rasmi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, zoezi la kupiga kura liendelee. Wataalamu, watendaji, leteni maboksi ya kura.

Waheshimiwa Wabunge ambao wako nje, waingie ndani. Mpiga kengele, piga kengele ili walioko kantini warudi ndani. Wakati kura zinahesabiwa tutaendelea na Muswada wa Sheria ya Pareto.

*(Hapa kengele ilipigwa ili Wabunge walioko nje ya Ukumbi wa Bunge waingie ndani)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, akidi yetu ni 324.

*(Hapa karatasi za kura ziligaiwa kwa Wabunge)*
*(Hapa Wabunge walipiha Kura ya Kuthibitisha Uteuzi wa Makamu wa Rais)*

**SPIKA:** Watakaokwenda kusimamia uchaguzi ni Katibu wa Bunge ambaye ndiye Msimamizi Mkuu, Mawakala wetu ni Mheshimiwa Hokororo na Mheshimiwa Agnesta, tunaomba mje msimame hapo mbele ya Siwa.

Kura zikusanywe. Nani hajapata karatasi ya kura?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mmeshatumbukiza?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Haya.

Waheshimiwa Wabunge, sasa niwatambue wageni wengine waliokuwepo Bungeni: Wageni wanne wa Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela, viongozi wa dini kutoka Kyerwa, Mkoani Kagera. *(Makofi)*

Wageni 12 wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, wafanyabiashara wa madini kutoka Mkoani Mara wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Sabuni Amani. *(Makofi)*

Wageni 18 wa Mheshimiwa Festo Sanga, viongozi na wachezaji wa timu ya mpira ya wavu wanawake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 44 wa Mheshimiwa Selina Kingalame, wanafunzi wa vyuo vikuu. *(Makofi)*

Wageni 147 wa Mheshimiwa Mwantumu Zodo. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, ni wanafunzi 26 na walimu watano wa Shule ya *Hosiana Daycare Centre* Dodoma.

Waheshimiwa wote mmepiga kura?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Haya funga maboksi. Kama tayari maboksi yaende ndani.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba mkae kuna ratiba nyingine.

Mheshimiwa Ndejembi unaitwa *lounge*, Mheshimiwa Ndejembi unaitwa *lounge*, unaitwa, unaitwa *lounge*.

Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge kaeni chini tafadhali.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba mkae. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Muswada, ninaomba mkae.

Waheshimiwa Wabunge, mnakumbushwa kuwa Ofisi ya Bunge imeandaa Tamasha la Michezo na Burudani *(Bunge Bonanza)* kwa udhamini wa *NMB* ambalo linatarajiwa kufanyika kesho siku ya Jumamosi, tarehe 29 Agosti, 2026, katika Viwanja vya Shule ya Sekondari ya John Merlini hapa Dodoma. Kauli mbiu ya Bonanza hilo ni pamoja na "*AFCON* 2027, Tanzania tupo tayari." Bonanza hili litawashirikisha Waheshimiwa Wabunge, watumishi wa Ofisi ya Bunge, Wizara, Taasisi za Umma, Vyuo Vikuu vilivyopo Dodoma na Vilabu vya Mazoezi Dodoma.

Bonanza hili litatanguliwa na matembezi yatakayoanza Chuo cha Mipango saa 12 asubuhi kuelekea Viwanja vya John Merlini. Baadhi ya michezo ya ushindani na burudani itakayofanyika ni pamoja na mpira wa miguu, mpira wa pete, mpira wa kikapu, mpira wa wavu, mbio, kuvuta kamba, kukimbiza

kuku, *draft* na kadhalika. Waheshimiwa Wabunge wote na Watumishi wa Bunge mnahimizwa kushiriki *Bonanza* hili.

Aidha, kufuatia shughuli za uapisho wa Mheshimiwa Makamu wa Rais mteule hapo kesho, Bunge litawakilishwa na wajumbe wa Kamati ya Uongozi, Kamati ya Nishati na Madini na Wabunge wa Mkoa wa Dodoma. Hivyo Waheshimiwa Wabunge wengine wote tunahimizwa kushiriki Bonanza hilo. Ahsanteni.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha Muswada unaopendekeza kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto, Sheria Na.1 ya Mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha hoja yangu, ninaomba nitumie nafasi hii kuungana na Wabunge wenzangu kumshukuru kwa dhati Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumwamini na kumteua kupitia CCM, Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Deogratius Ndejembi kuwa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliopata nafasi ya kuchangia hoja iliyowasilishwa hivi punde na Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Bungeni, kwamba uteuzi wa Mheshimiwa Ndejembi umezingatia uwezo na sifa zake za

uongozi, rekodi yake nzuri ya uchapakazi, nidhamu na uadilifu wake. Sina mashaka kwamba kura zilizopigwa hivi punde na sisi Wabunge, zitatosha na chenji itabaki. Nami niungane na wenzangu kumuahidi kutekeleza maelekezo ya viongozi wetu wote kwa sababu ndiyo wajibu wetu.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026.

Mheshimiwa Spika, lengo la kufutwa kwa sheria hii ni kuendeleza juhudi za Serikali za kupunguza gharama za uendeshaji kwa kuunganisha taasisi mbalimbali zinazotekeleza majukumu yanayofanana kwa lengo la kupunguza wingi wa taasisi za udhibiti kwa shughuli zinazofanana, kuimarisha uratibu, kuongeza ufanisi na kuhakikisha matumizi yenye tija ya rasilimali za umma katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu mbili ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi ikijumuisha jina la Muswada na fasili ya misamiati mbalimbali inayotumika katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inaweka masharti kuhusu kufutwa kwa Sheria ya Tasnia ya Pareto pamoja na masuala ya mpito ambapo majukumu, mali, madeni pamoja na Watumishi wa Bodi ya Pareto wanahamishiwa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Lengo la kufuta Bodi ya Pareto ni kupunguza wingi wa taasisi za udhibiti kwa shughuli zinazofanana, kuimarisha uratibu, kuboresha usimamizi na udhibiti, kuhakikisha matumizi yenye tija ya rasilimali za umma katika sekta ya kilimo yanakuwepo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, ninaomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026 ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na hatimaye kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHE. DANIEL GODFREY CHONGOLO (MB), WAZIRI WA KILIMO AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA TASNIA YA PARETO WA MWAKA 2026 KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA IJUMAA TAREHE 28 AGOSTI, 2026 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, ninaomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada unaopendekeza kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto, Sheria Na.1 ya Mwaka 1997.

**Mheshimiwa Spika**, ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kufutwa kwa Sheria hii ni kuendeleza juhudi za Serikali za kupunguza gharama za uendeshaji kwa kuunganisha taasisi mbalimbali zinazotekeleza majukumu yanayofanana kwa lengo la kupunguza wingi wa taasisi za udhibiti kwa shughuli zinazofanana, kuimarisha uratibu, kuongeza ufanisi na kuhakikisha matumizi yenye tija ya rasilimali za umma katika sekta ya kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Mbili ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya Utangulizi, ikijumuisha jina la Muswada na fasili ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Muswada inaweka masharti kuhusu kufutwa kwa Sheria ya Tasnia ya Pareto pamoja na masuala ya mpito, ambapo majukumu, mali, madeni pamoja na watumishi wa Bodi ya Pareto wanahamishiwa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Lengo la kufuta Bodi ya Pareto ni kupunguza wingi wa taasisi za udhibiti kwa shughuli zinazofanana, kuimarisha uratibu, kuboresha usimamizi na

udhibiti na kuhakikisha matumizi yenye tija ya rasilimali za umma katika sekta ya kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026 ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya kusomwa kwa mara ya Pili na hatimaye kuwa sehemu ya Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo haya, NAOMBA KUTOA HOJA.

Daniel G. Chongolo (Mb.)
**WAZIRI WA KILIMO**
28 Agosti, 2026

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono, Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, nichukue nafasi hii kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na tukio kubwa muda mfupi uliopita, la kupiga kura za kumuidhinisha Makamu wa Rais Mteule. Nitumie nafasi hii, kwanza kabisa kumpongeza kwa kuteuliwa kwa kushika nafasi hiyo na ni matumaini yangu Waheshimiwa Wabunge wote tutapiga kura nyingi zote za kumthibitisha kwenye

nafasi hiyo. Ni kijana ambaye anastahili na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uteuzi huo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026 kwa mujibu wa Kanuni ya 102(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2025.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026 uliosomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Tatu Kikao cha 58 kwenye Bunge la Kumi na Tatu Tarehe 26 Juni, 2026, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 100(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 139(14) na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, namna uchambuzi wa Muswada ulivyofanyika. Hatua za kufanya Muswada huu zilianza kwa maandalizi mbalimbali ya kiutendaji yaliyofanywa na Sekretarieti kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za Kamati. Maelezo ya uchambuzi wa Muswada uliofanywa na kuwasilishwa kwenye Kamati na Sekretarieti ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 25(2)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Hatua hii ilijenga msingi wa utekelezaji wa kazi za Kamati kuhusiana na Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 11 Agosti, 2026 ili kupokea maelezo ya Mheshimiwa Daniel Godfrey Chongolo, Waziri wa Kilimo kuhusu madhumuni na sababu za

Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo na Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika Ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 100(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya Mkutano na kusikiliza maoni ya wadau *(public hearing)* tarehe 12 na 13 Agosti, 2026 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Ninapenda kuwashukuru sana wadau wote waliotoa maoni yao kuuboresha Muswada huu akiwemo Ndugu Daniel Kapusi mkulima wa pareto.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia hoja zilizotokana na maelezo ya uchambuzi, maoni pamoja na nyaraka mbalimbali kuhusiana na Muswada huu. Mnamo tarehe 18 Agosti, 2026, Kamati ilikutana tena na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ili kujadili kuhusu hoja zilizobainika na kwa kila Ibara ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 100(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati iliitaarifu Ofisi ya Spika kwamba imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Muswada; Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026. Muswada huu umegawanyika katika Sehemu mbili na unapendekeza kufuta Sheria hii kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au dosari au kutatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Sheria hii kama zilivyoelezwa na mtoa hoja mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inajumuisha Ibara ya 1 na inataja jina la Sheria iliyokusudiwa kutungwa na Ibara ya 2 inayoeleza fasili ya maneno yaliyotumika katika Sheria hii. Sehemu ya Pili ya Muswada inafuta Sheria ya Tasnia ya Pareto na masharti ya mpito.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inahusu Ibara ya 3 – 8. Ibara ya 3 ya Muswada inafuta Sheria Na.1 ya Tasnia ya Pareto ya Mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Tasnia ya Pareto iliyofutwa ilitungwa mwaka 1997. Msingi wa kutungwa kwa Sheria hii ulielezwa na Waziri wa Kilimo na Ushirika wa wakati huo Mheshimiwa Dkt. Aaron D. Chiduo tarehe 28 Januari, 1997. Ninaomba kunukuu; "Mheshimiwa Spika sababu kubwa ya mabadiliko haya yanatokana na maamuzi yetu huko nyuma ambayo yanazingatia kutekeleza Sera za Serikali ya kujiondoa kabisa katika shughuli zote za biashara ili kutoa nafasi nzuri kwa taasisi za watu binafsi kuendesha biashara hizi, lakini pamoja na hilo, Muswada unakusudiwa kuweka mazingira mazuri ya wakulima, wasindikaji wenye viwanda, wauzaji na wanunuzi wa pareto kwa bidhaa zake na kuweza kuzifanya shughuli zao bila kuingiliwa sana na Serikali kama ilivyokuwa miaka ya nyuma na hivyo kuunda bodi ambayo itahusika zaidi na utoaji wa huduma muhimu kwa kuendeleza zao hili."

Mheshimiwa Spika, ninaishia nukuu yangu hapo. Taarifa inatokana na Taarifa Rasmi za Bunge ya tarehe 28 Januari, 1997.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sababu zilizoelezwa hapo juu za utungwaji wa sheria, lakini bado inaonekana zao hili halikulimwa kwa wingi kama ilivyotarajiwa. Ambapo takwimu zinaonesha kuwa wakulima wa pareto nchi nzima wapo takribani 12,500 na jumla ya ekari zinazolimwa ni 13,000 tu. Hivyo tathmini inaonesha kuwa Bodi ilikuwa na wigo mdogo wa usimamizi kwa sababu takwimu zinaonesha kuwa wakulima wa zao hili ni wachache, ukilinganisha na mazao mengine yanayosimamiwa na bodi mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, mathalan zao la korosho lina takribani wakulima 500,000 na ekari zinazolimwa ni takribani 2,000,000; zao la kahawa lina wakulima takribani 400,000 na ekari zinazolimwa ni 777,000; tumbaku ina wakulima takriban 150,000 na ekari zinazolimwa ni ekari 297,000; kahawa ina wakulima 450,000 na

ekari zinazolimwa ni ekari 741,000; na mkonge ina wakulima ni 50,000, ekari zinazolimwa ni 124,000.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kuongeza tija, kuboresha usimamizi wa udhibiti na kuhakikisha matumizi yenye tija ya rasilimali za umma Serikali inaona ifute Bodi ya Pareto na kuhamishia majukumu yake kwenye Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko *(COPRA)*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Serikali, Kamati ilionesha wasiwasi juu ya kulipeleka zao hili *COPRA* kwa kuwa Mamlaka hii inasimamia zaidi ya mazao 120. Hivyo, Kamati inaona ni vema kuweka mikakati mahsusi ya namna bora ya kulisimamia zao hili kutokana na upekee wake hata kama litahamishiwa kwenye Mamlaka ya *COPRA*.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii yanagusa mambo mengi, miongoni mwa mambo hayo ni kuhamisha majukumu, mamlaka na kazi zilizokuwa zinatekelezwa na Bodi ya Pareto kwenda katika Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko.

Mheshimiwa Spika, aidha, mkataba, leseni, kibali, hati na nyaraka nyingine ya Bodi ya Pareto itachukuliwa kuwa ni rejea ya Mamlaka. Vilevile, mali na madeni ambayo yalitokana na Bodi ya Pareto yatakuwa chini ya Mamlaka ya *COPRA*.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine yaliyojitokeza katika Muswada huu ni kuweka masharti katika leseni, kibali, idhini, cheti, usajili au ridhaa ambayo ilitolewa na Bodi ya Pareto kuwa itaendelea kutumika kana kwamba imetolewa na Mamlaka hii. Mashauri yoyote yaliyopo yataendelea kukamilishwa au kutekelezwa na Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuweka masharti kuwa watumishi waliokuwa wa Bodi ya Pareto wataendelea kuwa Watumishi wa Mamlaka. Aidha, Muswada huu unampa Waziri mamlaka ya kulichapisha katika Gazeti la Serikali kupitia *notice* na

kutangaza tarehe ambayo majukumu, mamlaka na kazi ambazo zinatekelezwa na Bodi zitahamishiwa kwenye Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni na ushauri wa Kamati, kwa sehemu kubwa Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Muswada uliowasilishwa na mtoa hoja. Hata hivyo, Kamati ina maoni na ushauri ambao ni vema Serikali ikauzingatia na kuufanyia kazi kwa kuwa ni masuala yanayohusisha zao la pareto kama ifuatavyo:-

(i) Ianzishwe kurugenzi itakayojitegemea ndani ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko *(COPRA)* itakayoratibu ubora, masoko na maendeleo ya mnyororo wa thamani ya pareto. Hii inatokana na ukweli kuwa zao la pareto ni zao la kipekee, ni zao la mkakati kwa Tanzania na kwa kuzingatia mchango wake katika uchumi na nafasi muhimu ambayo Tanzania inaishikilia katika uzalishaji wa pareto duniani, Tanzania inashikilia nafasi ya pili kwa uzalishaji ikiwa baada ya Tasmania. Bado Kamati inaona ni muhimu kuendelea kulinda, kuendeleza na kuimarisha zao la pareto nchini;

(ii) Serikali ihakikishe inalinda na kuhifadhi maslahi ya watumishi waliokuwa wa Bodi ya Pareto ambao wataendelea na ajira zao chini ya Mamlaka wa Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko, haki hiyo izingatie haki na stahiki zao za msingi na za kiutumishi; na

(iii) Serikali ihakikishe inatoa elimu na uelewa wa kutosha kwa wadau na walengwa wa mabadiliko haya ya sheria hususan kuhusu kufutwa kwa Bodi ya Pareto na majukumu yake kuhamishiwa kwenye Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko *(COPRA)*. Elimu hiyo itasaidia kuwawezesha wadau kuelewa mabadiliko hayo, majukumu ya taasisi zinazoathiri majukumu hayo pamoja na taratibu na huduma watakazopaswa kuzifuata baada ya mabadiliko hayo ili

kuhakikisha utekelezaji wa sheria mpya unakuwa na ufanisi na haileti mkanganyiko kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, ninaomba kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia Muswada huu, ninaomba niwatambue kama walivyoorodheshwa kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Daniel Godfrey Chongolo, Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri wa Kilimo kwa ushirikiano mkubwa walioipa Kamati na wanaoendelea kuipa Kamati. Kwa sehemu kubwa umechangia kuwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia Watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bwana Gerald Geofrey Mweli akisaidiwa na Naibu Makatibu Wakuu: Profesa Peter Msoffe na Ndugu *Engineer* Athumani Kilundumya.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninamshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa kuwaongoza vyema Watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na jedwali la marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**28 AGOSTI, 2026**

# MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA TASNIA YA PARETO WA MWAKA 2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, ninaomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kuhusu Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025,

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026 ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Tatu, Kikao cha 58 kwenye Bunge la Kumi na Tatu, tarehe 26 Juni, 2026 kwa mujibu wa Kanuni ya 99(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 100 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 139 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Ninaomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.2 Namna Uchambuzi wa Muswada ulivyofanyika

**Mheshimiwa Spika**, hatua za kuufanya muswada huu zilianza kwa maandalizi mbalimbali ya kiutendaji yaliyofanywa na Sekretarieti kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za Kamati. Maelezo ya uchambuzi wa muswada ulifanywa na kuwasilishwa

kwenye Kamati na Sekretarieti ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 25(2)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Hatua hii ilijenga msingi wa utekelezaji wa kazi za Kamati kuhusiana na Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 11 Agosti, 2026 ili kupokea maelezo ya Mhe. Daniel Godfrey Chongolo, (Mb) Waziri wa Kilimo kuhusu madhumuni na sababu za Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 100(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearing*) tarehe 12 na 13 Agosti, 2026 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, ninapenda kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu akiwemo Daniel Kapusi-Mkulima wa Pareto

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia hoja zilizotokana na maelezo, uchambuzi, maoni pamoja na nyaraka mbalimbali kuhusiana na muswada huu. Mnamo tarehe 18 Agosti, 2026 Kamati ilikutana tena na Waziri wa Kilimo ili kujadiliana kuhusu hoja zilizobainika kwa kila ibara ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 100 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na Kamati iliitaarifu Ofisi ya Spika kwamba imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026. Muswada huu umegawanyika katika sehemu Mbili (2) na unapendekeza kufuta sheria hii kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au dosari au

kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hii kama zilivyoelezwa na mtoa hoja mbele ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inajumuisha **Ibara ya 1** na inataja jina la Sheria inayokusudiwa kutungwa na **Ibara ya 2** inayoeleza fasili ya maneno yaliyotumika katika sheria hii.

**2.1 Sehemu ya Pili ya Muswada inafuta Sheria ya Tasnia ya Pareto na Masharti ya Mpito.**

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inahusu Ibara ya 3 mpaka 8. Ibara ya 3 ya Muswada inafuta Sheria Na.1 ya Tasnia ya Pareto ya Mwaka 1997.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Tasnia ya Pareto inayofutwa, ilitungwa Mwaka 1997. Msingi wa kutungwa kwa sheria hii ulielezwa na Waziri wa Kilimo na Ushirika wa wakati huo Mheshimiwa Dkt. Aaron D. Chiduo tarehe 28 Januari, 1997 ninaomba kunukuu;
**"**Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya mabadiliko haya yanatokana na maamuzi yetu huko nyuma ambayo yanazingatia kutekeleza sera ya Serikali ya kujiondoa kabisa katika shughuli zote za biashara ili kutoa nafasi nzuri kwa taasisi na watu binafsi kuendesha biashara hizo. Lakini pamoja na hilo muswada unakusudia kuweka mazingira mazuri ya wakulima, wasindikaji, wenye viwanda, wauzaji na wanunuzi wa pareto kwa bidhaa zake na kuweza kuzifanya shughuli zao bila kuingiliwa sana na Serikali kama ilivyokuwa miaka ya nyuma na hivyo kuunda Bodi ambayo itahusika zaidi na utoaji wa huduma muhimu kwa kuendeleza zao hilo" (Taarifa rasmi za Bunge tarehe 28 Januari 1977).

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na sababu zilizoelezwa hapo juu za utungwaji wa sheria hii lakini bado inaonekana zao hili halikulimwa kwa wingi kama ilivyotarajiwa ambapo takwimu zinaonyesha kuwa wakulima wa Pareto nchi nzima wapo takribani 12,500 na jumla ya ekari 13,000 tu zinalimwa. Hivyo tathmini inaonyesha kuwa Bodi ilikuwa na wigo mdogo wa usimamizi kwa sababu

takwimu zinaonesha kuwa Wakulima wa zao hili ni wachache ukilinganisha na mazao mengine yanayosimamiwa na Bodi mbalimbali nchini. Mathalani zao la Korosho lina takribani wakulima 500,000 na ekari zinazolimwa ni takribani 2,000,000, Kahawa wakulima takribani 400,000 na ekari 778,000, Tumbaku Wakulima takribani 150,000 na ekari 297,000, Kahawa wakulima 450,000 na ekari 741,000 na Mkonge wakulima 50,000 na ekari 124,000.

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuongeza tija, kuboresha usimamizi wa udhibiti na kuhakikisha matumizi yenye tija ya rasilimali za umma, Serikali inaona ifute Bodi ya Pareto na kuhamishia majukumu yake kwenye Mamlaka ya udhibiti wa Nafaka na Mazao mchanganyiko (COPRA).

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na nia njema ya Serikali, Kamati ilionesha wasiswasi juu ya kulipeleka zao hili COPRA kwa kuwa Mamlaka hii inasimamia zaidi ya mazao 120 hivyo Kamati inaona ni vema kuweka mikakati mahsusi ya namna bora ya kulisimamia zao hili kutokana na upekee wake.

**Mheshimiwa Spika,** Marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii yanagusa mambo mengine. Miongoni mwa mambo hayo ni kuhamisha majukumu, mamlaka na kazi zilizokuwa zinatekelezwa na Bodi ya Pareto kwenda katika Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko.

Aidha, Mkataba, Leseni, Kibali, Hati au Nyaraka nyingine ya Bodi ya Pareto itachukuliwa kuwa ni rejea ya Mamlaka na vile vile mali na madeni ambayo yalikuwa yamekabidhiwa au yalitokana na Bodi ya Pareto yatakuwa chini ya Mamlaka**.**

**Mheshimiwa Spika,** mambo mengine yaliyojitokeza katika muswada huu ni kuweka masharti katika leseni, kibali, idhini, cheti, usajili au ridhaa ambayo ilitolewa na Bodi ya Pareto kuwa itaendelea kutumika kana kwamba imetolewa na Mamlaka na mashauri yalipo yataendelezwa, kukamilishwa au kutekelezwa na Mamlaka.

**Mheshimiwa Spika,** jambo jingine ni kuweka masharti kuwa Watumishi waliokuwa wa Bodi ya Pareto wataendelea kuwa watumishi wa Mamlaka. Aidha, Muswada huu unampa mamlaka Waziri ya kuchapisha katika Gazeti la Serikali kupitia notisi, na kutangaza tarehe ambayo majukumu, mamlaka na kazi ambazo zinatekelezwa na Bodi ya Pareto zitahamishiwa rasmi kwenye Mamlaka.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na mtoa hoja. Hata hivyo Kamati ina maoni na ushauri ambao ni vema Serikali ikauzingatia na kuufanyia kazi kwa kuwa ni masuala yanayohusiana na zao la pareto kama ifuatavyo;-

a) Kuanzisha Kurugenzi inayojitegemea ndani ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) itakayoratibu uzalishaji, ubora, masoko na maendeleo ya mnyororo wa thamani ya pareto. Hii inatokana na ukweli kuwa zao la pareto ni la kipekee na la kimkakati kwa Tanzania, kwa kuzingatia mchango wake katika Uchumi na nafasi muhimu ambayo Tanzania inashikilia katika uzalishaji wa Pareto duniani, ambapo inashikilia nafasi ya pili jambo linaloonesha umuhimu wa kuendelea kulinda, kuendeleza na kuimarisha Tasnia ya Pareto Nchini.

b) Serikali ihakikishe inalinda na kuhifadhi maslahi ya watumishi waliokuwa wa Bodi ya Pareto ambao wataendelea na ajira zao chini ya Wakala wa Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Haki hiyo izingatie haki na stahili zao za msingi za kiutumishi.

c) Serikali ihakikishe inatoa elimu na uelewa wa kutosha kwa wadau na walengwa wa mabadiliko haya ya sheria, hususan kuhusu kufutwa kwa Bodi ya Pareto na Majukumu yake kuhamishiwa kwenye Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA).

Elimu hiyo itasaidia kuwawezesha wadau kuelewa mabadiliko hayo, majukumu ya taasisi zitakazoathiri majukumu hayo, pamoja na taratibu na huduma watakazopaswa kuzifuata baada ya mabadiliko hayo ili kuhakikisha utekelezaji wa sheria mpya unakuwa na ufanisi na haileti mkanganyiko wa wadau

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, ninapenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, ninaomba niwatambue kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb | **M/Mwenyekiti** |
| 3. | Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Tauhida Galos Cassian, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Omar Marcus Msigwa, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Kabula Enock Shitobelo, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Dkt. Ritta Enerpher Kabati, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Magreth Baraka Ezekiel, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Abubakar Alli Omari, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Kenneth Ernest Nollo, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Khalfan Issa Mohamed, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Khamis Hamad Yussuf, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Amour Seif Abdalla, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Khalid Mussa Nsekela, Mb | Mjumbe |

22. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb Mjumbe
23. Mhe. Salum Khamis Salum, Mb Mjumbe
24. Mhe. Dickson Nathan Lutevele Villa Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninapenda kumshukuru Mhe. Daniel Godfrey Chongolo (Mb) - Waziri wa Kilimo na Mhe. David Ernest Silinde (Mb) – Naibu Waziri wa Kilimo, kwa ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati ambao kwa sehemu kubwa umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kikamilifu.

Ninawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Gerald Geofrey Mweli, akisaidiwa na Naibu Makatibu Prof. Peter Msoffe na Ndg. Athumani Kilundumya

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee ninamshukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Baraka I. Leonard kwa kuwaongoza vyema watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Deodatus Philip Mwanyika (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**
28 Agosti, 2026

**SPIKA:** Ahsante. Wajumbe kabla sijamwita Katibu niwatambulishe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi 12 waliokuja kushiriki kwenye *Bonanza* kutoka Zanzibar. Karibuni sana. *(Makofi)*

Ninaomba *Sergeant-at-Arms* upige kengele Wabunge wote warudi ndani. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MATOKEO YA KURA YA UTHIBITISHO WA MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutangaza matokeo ya kura ya kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais, matokeo haya ninayatangaza kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 50(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jina lililopendekezwa ni la Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, jumla ya kura zilizopigwa zilikuwa 324, idadi ya kura zilizoharibika sifuri, kura hapana sifuri, idadi ya kura halali ni 324. Hivyo, ninapenda kutoa taarifa kuwa uteuzi wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umethibitishwa na Bunge kwa kura 324 sawa na 100%. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, matokeo haya yamezidi 50% ya Wabunge wote kama inavyoelekezwa katika Ibara ya 50(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni, Katibu ndiye anayetangaza matokeo na ameshatangaza matokeo inawezekana wengine hamkusikia au mmeshangaa. Kwa hiyo, kura zilizopigwa ni 324, kura zilizoharibika sifuri, idadi iliyopiga ni 324, kura za hapana sifuri kama alivyosema Katibu. Kwa hiyo, jumla ya ushindi wa Mheshimiwa Makamu wa Rais wetu ni 324, sawa na 100%.

Waheshimiwa Wabunge, jana nilipata salamu kutoka kwa baadhi ya Mabalozi wengi wa nchi hii ambao wako Tanzania, ambao kwa kweli wameridhika na uteuzi wa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, Bunge leo tarehe 28 Agosti, 2026 limemthibitisha Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi kuwa Makamu wa Rais wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba. *(Makofi)*

Hongera sana. Sasa karibu kama una maneno mawili matatu baadaye tukuage maana humu ndani utakuwa huingii tena, karibu. *(Makofi/Vigelegele)*

**MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI – MAKAMU WA RAIS MTEULE WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninapenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha kuweza kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa shukrani zangu za dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za dhati zinaanza kwenda kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani aliyoionesha kwangu si tu katika uteuzi huu wa kuwa msaidizi wake namba moja kama Makamu wake wa Rais, lakini imani yake aliyoiweka kwangu kwa kuanza kuniteua kunipeleka Ofisi ya Rais (TAMISEMI), kwa kuniteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), kwa kuniteua kuwa Waziri wake wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na mwisho kabisa kwa kuniteua kuwa Waziri wa Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni imani kubwa sana Mheshimiwa Rais ameionesha kwangu kwa kunipa dhamana hii ya kuwa msaidizi wake yaani Makamu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamezungumza hapa wengi juu ya wanavyonifahamu, juu ya Mheshimiwa Rais kupenda kufanya kazi na vijana na kuwapatia dhamana, lakini ninafahamu kwamba ukubwa wa dhamana hii haitopimwa kwa ujana wangu peke yake, wala haitopimwa kwa ujana wangu kabisa. Dhamana hii itapimwa kwa utii kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania. Dhamana hii itapimwa kwa uadilifu kwa Watanzania, dhamana hii itapimwa kwa kazi yoyote nitakayotumwa na Mamlaka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuitekeleza katika nafasi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani zingine za kipekee nizipeleke kwa Chama changu, Chama Cha Mapinduzi (CCM). Kwa maana uteuzi wangu, majina yalijadiliwa Kamati Kuu, nikapendekezwa Kamati Kuu, jina likapelekwa *NEC*, Wajumbe wa *NEC* wakaridhia niweze kuwa msaidizi namba moja wa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama Makamu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imani ile ya Chama Cha Mapinduzi walioionesha Wajumbe wa Halmashauri Kuu ni imani kubwa, lakini si imani kubwa kwa Deo Ndejembi peke yake ni imani ambayo inaonesha ni namna gani Chama Cha Mapinduzi kinalea vijana, kinawaamini vijana na kuwapika vijana ili kuweza kushika dhamana mbalimbali katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimekulia ndani ya Chama Cha Mapinduzi, nimezaliwa CCM, nimekulia CCM, nimepata bahati ya kuhudumu kama kiongozi ndani ya CCM, kuanzia Baraza Kuu la Umoja wa Vijana Taifa 2008 – 2012 na baadaye Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM nikiwakilisha vijana 2012 – 2017; baadaye kuaminika katika Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, kuwa Mkuu wa Wilaya, Mbunge, Naibu Waziri, Waziri na leo sasa nafasi niliyosimama hapa kushukuru kuthibitishwa na Bunge hili kwenda kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia ninafahamu nafasi hii si ya mtu mmoja, ni ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nafasi hii ni ya Watanzania, leo ninakwenda kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama Makamu wake. Ninakuwa ni Makamu wa Rais wa wana-Njombe anakotoka Mheshimiwa Sigrada, ambaye ni wa chama kingine, wana-Tunduru anakotoka rafiki yangu Mheshimiwa Ado Shaibu, ambaye ni wa chama kingine, kwa Mheshimiwa Singo.

Mheshimiwa Spika, Ninakuwa Makamu wa Rais siyo wa Wana-CCM peke yake, ninakuwa Makamu wa Rais wa Watanzania wa vyama vyote, kama Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Watanzania wa vyama vyote. Nitajitahidi kwa unyenyekevu mkubwa sana kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa kiungo kwa Watanzania wote, kama mapenzi yake yatakavyotaka kwa sababu, ninafanya kazi chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee ninatoa shukrani zangu za dhati kwako, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu na Bunge lako Tukufu. Kwa Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge na bila ya kuwasahau Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani hizi ninazozitoa kwako na kwa Bunge lako Tukufu, siyo tu kwa sababu ya kura zote nilizozipata leo hapa ndani, lakini ni kwa sababu ya malezi uliyonipatia wewe pamoja na Bunge lako kutokea kipindi ninaingia kuwa Mbunge, mwaka 2020. Pia, kwa Wabunge wenzangu kwa namna tulivyoshirikiana katika mambo mbalimbali bila kuangalia vyama vyetu. Nimesimama hapa mara nyingi kujibu maswali, kama Naibu Waziri; nimesimama hapa kuwasilisha bajeti; yote hiyo ni ndani ya Bunge lako Tukufu na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee ninashukuru kwa kura nilizozipata leo humu ndani. Kwanza, imeashiria ya kwamba, mna imani na Dkt. Samia Suluhu Hassan na uteuzi alioufanya. Pili, inaashiria kwamba, mna imani na mimi, lakini siyo tu imani na mimi, imani hiyo imejengwa na kuzaliwa kwa kuishi nanyi kama wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waswahili wanasema ukikopeshwa utu, lipa kwa utu; ukikopeshwa wema, lipa kwa wema. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amenikopesha utu, amenikopesha wema na nitamlipa kwa utu na wema kwa kuwa mtiifu kwake. Pia, Bunge lako Tukufu kwa kura nilizopata leo, mimi nikopeshe imani na nitailipa imani hiyo kwa kutekeleza majukumu yangu

kadiri Mungu atakavyonibariki, ili niweze kufikia yale malengo aliyonayo Rais wangu na ninyi Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa malezi yake nilipokuwa nikifanya chini yake, kama Waziri wake, ambaye yeye ana dhamana ya kunisimamia kwa sababu, ndiyo kiongozi wa Serikali. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mwigulu Nchemba na ninatarajia kuendelea kupata ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yangu. Pia, nina imani ushirikiano utakuwa mkubwa na mwananchi mwenzangu vilevile. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninazungumza ya mwananchi, nikakuona kama unataka kuwasha *mic!* Ninaona niendelee.

**SPIKA:** Kuna maneno mengine tutayatoa kwenye *Hansard*. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI – MAKAMU WA RAIS MTEULE WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Mawaziri wote kwa namna ambavyo tumefanya kazi kwa pamoja, kwa umoja, kwa mshikamano, kwa kushirikiana kama ndugu katika kuhakikisha tunamsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutimiza malengo aliyonayo kwa Watanzania. Ninawashukuru Waheshimiwa Naibu Mawaziri wote kwa ushirikiano mkubwa ambao tumekuwanao wakati wote, lakini kipekee ninamshukuru Mheshimiwa Salome Wycliff Makamba, Naibu Waziri wa Nishati, kwa kazi ambayo anaifanya na kwa usaidizi wake aliokuwa ananipatia. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Makamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mara zote, hata usiku wa manane, nilipokuwa ninampigia, kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali, amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha tunamsaidia Rais wetu kufikia malengo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeweka mwisho, siyo kwamba, siyo muhimu, lakini ninawashukuru Wananchi wa Jimbo la Chamwino kwa imani waliyonipatia ya kuwatumikia, kama Mbunge wao, kwa kipindi hiki cha pili ambacho ninaenda kukihitimisha. Amezungumza Mheshimiwa Bashe, nimeomba dhamana mara ya kwanza; sijasema mimi Mheshimiwa Sigrada, ni aliyoyasema Mheshimiwa Bashe yalipotokea, bado wana-Chamwino wameendelea kuwa na imani nami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata niliporudi mara ya pili kwenda kuomba dhamana, imani ile ya Wana-Chamwino ilithibitika baada ya kuwa nimechangiwa mafuta na Mheshimiwa Simbachawene. Pia, nasema hata Mheshimiwa Waziri Mkuu amewahi kunichangia katika kipindi hicho. Hata kipindi ninaachia ukuu wa wilaya Mheshimiwa Mavunde na yeye alinipatia gari lake, kwa ajili ya kampeni, lakini wameonesha imani kubwa na kunichagua. Baada ya miaka mitano imani ile imeendelea, wakanichagua tena kuwa Mbunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wana-Chamwino, akiwemo kaka yangu Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mbunge pacha wa Wilaya ya Chamwino, ninawaahidi ya kwamba, mimi bado ni mwana-Chamwino na kwa sababu Kigogo kimeongewa kwa mara ya kwanza Bungeni na Mheshimiwa Profesa Kabudi, nitawaambia Wana-Chamwino kwamba, *ane ngh'ali nilimyenyu, mlece lema nonjela ng'hani yoyose iliya hamba mkusaka niwatazaje*. Nimezungumza maneno haya kwamba, mimi bado ni Mwana-Chamwino na kwa jambo lolote lile wasisite wakati wowote ule kunijulisha na tutashirikiana kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, ninawaomba tushikamane, tuweze kuhakikisha Watanzania wanapata yale wanayoyahitaji. Kwa maana Mheshimiwa Rais wetu ametoa fedha nyingi katika miradi mbalimbali, wajibu wetu ni kusimamia, kuhakikisha kwamba, huduma zile zinafika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi ninashukuru tena kupata fursa hii ya kuzungumza mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwaaga rasmi na kusema nitawakumbuka sana.

Ahsanteni sana kwa undugu tuliokuwanao. Ninashukuru sana, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa, Mheshimiwa Makamu wa Rais, kwa heshima na taadhima na sisi tunashukuru kwa ushirikiano uliotupa, ukarimu na ubinadamu wako ndani ya Bunge hili. Kwa kweli, sifa hii ni kubwa sana kwako, endeleanayo na Mungu atakusaidia kumsaidia Rais kuendesha Taifa letu. *(Makofi)*

Sasa, ninakuruhusu uende kwenye majukumu mengine. Siyo kwenye kiti.

*(Hapa Mhe. Deogratius J. Ndejembi - Makamu wa Rais Mteule wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Alitoka Ukumbini)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. *(Makofi)*

Ahsanteni. Waheshimiwa Wabunge tumeona urahimu wa Makamu wa Rais. Kaja *personal* kuwashukuru wapinzani na ametaja jina la Mheshimiwa Sigrada, maana ndiye alikuwa anaongoza mapambano ya kura za ndiyo leo, hongereni sana. Hiyo ndiyo Tanzania anayoitaka Mama Samia. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa ninaongeza muda mpaka tutakapomaliza shughuli yetu ya leo. Sasa, tunaanza kuchangia.

**Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kabati! Kama hauna mchango, unasema sina, unakaa. *(Kicheko)*

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, ili niweze kuchangia muswada ambao upo mbele yetu. Kwanza kabisa ninaomba nimshukuru Mwenyenzi Mungu, lakini kabla sijaanza mchango wangu na mimi ninaendelea kuwapongeza Wabunge wote ambao leo hii

tumepigia Makamu wa Rais Mteule kura zote za ndiyo kwa 100%. Hongereni sana Wabunge wote humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri wa Kilimo, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kutuletea huu muswada. Vilevile, ninampongeza Mwenyekiti wa Kamati yetu, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, kwa kazi nzuri, ambayo ameifanya na Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipoletewa huu muswada tulipata shida kidogo kwa sababu, unakwenda kufuta Sheria ya Zao la Pareto. Zao hili linapelekwa *COPRA,* sehemu ambayo tayari imeanza uangalizi wa mazao 120; tulipata shida kidogo, ukizingatia kwamba, zao la pareto lina upekee wake. Kwanza kabisa, zao hili Tanzania lina mchango mkubwa sana, ni la pili duniani kiuchumi kwa hiyo, tulikuwa tunaona kwamba, ni kwa nini zao hili lipelekwe kuchanganywa kwenye mazao mengi? Tukapata wasiwasi mkubwa!

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati. Tunawashukuru sana hata wanasheria wa Bunge, waliweza kutuelimisha tukajua sheria vizuri na tukaona ipo haja sasa hili zao kweli, lipelekwe *COPRA*.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, yapo mambo ambayo tuliona yaangaliwe; kwanza, tuliomba iundwe kurugenzi kwa zao hili tu kwa sababu, likienda kuchanganywa kwenye mazao mengine bado halitapewa kipaumbele. Kwa hiyo, tuliomba hii kurugenzi ihakikishe kwamba, zao hili linaangaliwa kwa ukaribu na uzalishaji wake uongezeke kwa sababu, wakulima wa zao hili ni 12,500 tu Tanzania nzima linazalishwa ekari 13,000 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaona kwamba, upo uwezekano Tanzania yetu, na sisi kama tutaweza, kuhamasisha wakulima wengi wazalishe zao hili la pareto tuweze hata kuwa wa kwanza Duniani kwenye kuzalisha zao hili. Kwanza ni zao ambalo linatengeneza viuatilifu ambavyo ni *organic* kwa hiyo, ni zao

ambalo tunategemea kwamba, litatusaidia kiuchumi kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninakubaliana na hoja iliyoletwa Mezani na kuwahamasisha Wabunge wote kwamba, turidhie huu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya zao hili la pareto. Tunaiomba Serikali iendelee kutoa elimu kubwa kwa wakulima, lakini pia, iendelee kuangalia maeneo ambayo yanakubali hili zao la pareto. Wakulima waelimiswe umuhimu wa zao hili na vilevile, uwepo mkakati maalum kwamba, wale wakulima wa hili zao wapatiwe pembejeo, kama ambavyo bodi iliyokuwepo ilikuwa inafanya. Pia, tulikuwa na kiwanda kimoja cha zao hili pale Mufindi, sasahivi tuna viwanda viwili, kimoja kipo kule Mbeya.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Yustina. Mheshimiwa Khadija Aboud na Mheshimiwa Dickson wajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa, na mimi nafasi, kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Tasnia ya Pareto ya Mwaka 2026.

Mheshimiwa Spika, ninapongeza sana kwa kitendo tulichotoka kumaliza sasahivi, cha kumpa kura zote Makamu wa Rais. Tunamuombea kwa Mungu ampe nguvu, utashi na hekima, ili aweze kutimiza majukumu yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema kwamba, muswada huu ni wa kwenda kufuta Sheria Na. 1 ya Pareto, ya Mwaka 1997, hasa kwenye Ibara ya 3 na ya 8; Sheria ambayo imewahi kuunda Bodi ya Pareto. Bodi ya Pareto iliundwa mahsusi, kwa ajili ya kusimamia zao hili kwenye kuendeleza ukuaji, kudhibiti ubora na kusimamia mnyororo mzima wa thamani, ikiwa ni pamoja na masoko. Vilevile, kutekeleza azma na sera ya kuitoa Serikali katika biashara,

ili zao hili lipewe watu binafsi na na bodi iweze kulisimamia kwa ukaribu.

Mheshimiwa Spika, zao la pareto ni zao pekee, kwa maana kwamba, kwanza ni zao la kimkakati katika nchi ya Tanzania linalotegemewa kwa uchumi na kupata fedha za kigeni. Vilevile, ni zao ambalo limewahi kutupa heshima kubwa sana kwa sababu, Tanzania ni nchi ya pili duniani kwa uzalishaji wa pareto iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni zao ambalo linafanya vizuri katika kutengeneza viuatilifu au viuadudu, ambavyo ni asili *(natural organic compound)*. Sasahivi kutokana na uchache wa pareto, watu wanatengeneza viuatilifu kwa kutumia kemikali; kemikali hizi zina mabaki *(residue)* ambayo yana athari kwa wakulima, kwa walaji, kwa Watanzania na pia, si rafiki kwa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona kwamba, viuatilifu vinavyotengenezwa na zao la pareto vinatumika nyumbani, ni hizi *spray* zinazotumika, kwa ajili ya mbu, mchwa na nzi kwa sababu, havina athari ya moja kwa moja kwa binadamu. Ni viuatilifu vizuri sana vya kuhifadhi mazao *store*, ukilinganisha na hivi vya kemikali ambavyo wakati mwingine, kwa mfano kwenye mahindi yule dumuzi, vimeshindwa kumdhibiti. Ni viuatilifu vizuri sana vya kuogesha mifugo, *acaricide* nzuri zote zina *pyrethrin*. Kwa hiyo, tunavyoenda kujadili lazima tuone kwamba, kuna *attention* ambayo Wizara inatakiwa kuiweka katika zao hili.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapoenda kulihamishia zao hili kwenye Mamlaka ya Udhibiti na Mazao Mchanganyiko *(COPRA)*, sisi tunaomba kupendekeza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni, zao hili linazalishwa kwa takribani tani 2,200. Sasahivi linavyoenda *COPRA*, *COPRA* ihakikishe kwamba, uzalishaji wa zao hili unaongezeka kwa sababu, matumizi yake ni muhimu na ni mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili iweze kusimamia tunaiomba *COPRA* iweke kurugenzi yenye watu waliobobea katika zao la pareto,

ikiwa ni pamoja na kuwahamisha wale ambao walikuwa kwenye Bodi ya Pareto, wenye uzoefu. Wanaweza wakahamia huku pamoja na maslahi yao na kupendekeza wengine, lakini ndani yake iweke mfumo mzuri sana wa maafisa ugani, ambao wataweza kusimamia zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzalishaji si kwa ajili ya *export* tu katika zao hili, lakini ni pamoja na Watanzania ambao sasa wame-*shift* kwenda kuzalisha mazao, ambayo yanaitwa ya kiekolojia, mazao ambayo yanauzwa kwa bei ya juu kwenye hoteli za kitalii na *supermarket*. Haya mazao ndiyo ambayo yanahitajika Tanzania, tuyatumie wenyewe, kwa ajili ya afya zetu, ukizingatia sasahivi kuna magonjwa mengi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. Ninaungana na Serikali kwamba, bodi hii ifutwe na majukumu yake yahamishiwe *COPRA*, lakini kwa kuzingatia kwamba, kurugenzi iendelee kufanya kazi. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Khadija Aboudi, jiandae Mheshimiwa Dickson, jiandae Mheshimiwa Kenneth.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais wetu kwa kura nyingi za kishindo na ushindi alioupata hii leo. Ni imani yetu, sisi Watanzania tunamuamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba na mimi nichangie kwenye Muswada ulioko mbele yetu wa tasnia ya pareto. Ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao mkubwa na mzuri waliotupa katika

kufanikisha jambo hili na Muswada huu uko hapa Bungeni sasa tunaujadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhumuni la kuundwa kwa bodi na Sheria hii ya Pareto mwaka 1997, ilikuwa ni kulinda, kuendeleza, kuweka mazingira mazuri ya wakulima, wasindikaji, wenye viwanda, wauzaji, wanunuzi wa pareto, pamoja na kutoa huduma muhimu kwa kuendeleza zao hili. Bodi ya Pareto shughuli zake zote sasa zinakwenda kuchukuliwa na *COPRA*, ambayo ni Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko katika dhumuni lilelile la kuhakikisha kuwa, zao hili linakuwa na ubora, linakuwa na soko, linalindwa na kuendelezwa, kwa kuzingatia kwamba, ni zao la kipekee na la kimkakati.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Tanzania ni nchi ya pili kwa uzalishaji Duniani, lakini hapohapo, Dunia nzima zao hili linazalishwa na nchi nne tu. Nchi ya kwanza ni Australia kule Tasmania, nchi ya pili ni Tanzania, nchi ya tatu ni Kenya na nchi ya nne ni Rwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zao hili linaonekana kwamba, ni muhimu na la kimkakati kwa sababu, sasa viwanda vingi duniani vinatengeneza kemikali, kwa ajili ya kutengeneza dawa, ambapo kemikali zile zina sumu na zinahatharisha afya zetu. Zao la pareto ni *natural* na *organic* kwa dawa zetu, siyo zile dawa zinazotengenezwa kiwandani ki-*scientistic*.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu huo ninaendelea kusisitiza kwamba, zao hili lipelekwa kwenye bodi ya *COPRA*, ambayo ina mchanganyiko wa mazao mengi na yataendelea kuongezeka. Sasahivi yako zaidi ya 120, halafu tunapeleka na zao hili la kimkakati; ndipo tunasema kwamba, kwa mamlaka hii ya udhibiti *(COPRA)*, ambayo itakwenda kusimamia zao hili sasa, tunaomba iwekwe bodi maalumu, ambayo itasimamia kwa ukaribu zaidi juu ya kuliendeleza zao hili katika uzalishaji, kutafuta soko na kuongeza mnyororo wa thamani, ili Tanzania badala ya kuwa namba mbili tuwe namba moja. *(Makofi)*

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Aboud. Ahsante, malizia.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dickson. Wajiandae Mheshimiwa Kenneth na Mheshimiwa Dkt. Pindi.

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Bodi ya Pareto. Ninaomba nielekee moja kwa moja kwenye hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninaomba ieleweke kwamba, ninaunga mkono hoja ya kuifuta Bodi ya Pareto na kuhamishia majukumu yake kwenye *COPRA*. Kwa nini ninafanya hivyo?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Tanzania inashika namba mbili kwa uzalishaji duniani, lakini bado kiwango cha uzalishaji si cha kuridhisha ukilinganisha na mahitaji halisi ya viwanda vya kusindika pareto. Kwa mujibu wa taarifa nilizonazo, kwa sasa, wazalishaji wa pareto kwa mwaka mzima wanazalisha tani 3,800 ilihali mahitaji ya viwanda na usindikaji ni tani 9,000. Hii inaonesha kwamba, zipo sababu mbalimbali zinazosababisha kutofikiwa kwa malengo haya ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, sasa, pamoja na kuunga mkono hoja hii na kupeleka zao hili *COPRA*, ninaomba niishauri Serikali kwamba, huku tunakolipeleka ni lazima tuwe na mpango mkakati wa kuhakikisha kuwa linaendelea kuwa bora. Kwa nini tuwe na mpango mkakati?

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu, zipo changamoto ambazo zimesababisha bodi kutokufikia malengo. Changamoto hizo ni pamoja na bei ndogo ya kununua maua ya pareto, ambayo imesababisha wakulima kukata tamaa katika kuhudumia zao hili. Kwa hiyo, *COPRA* ni lazima waje na mpango wa kuhakikisha kwanza wanaboresha soko.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni ubora wa pareto. Kilichoangusha soko la pareto yetu ni ubora wake unaotokana na mbegu. Ninaomba niishauri Serikali, itakapoipeleka huko isije ikawa *business as usual;* kwamba, wamechukua zao, wameliingiza *COPRA,* lakini bado wanatumia mifumo ileile, itakuwa hakukuwa na haja ya kuivunja bodi. Tutakachokuwa tumeepuka ni gharama tu, lakini kile kiwango cha ubora wa pareto, kwa maana ya ile sumu inayopatikana kwenye yale maua, kuna *factor* nyingi sana mle ndani ikiwemo ubora wa mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo jambo lingine ambalo limesababisha zao letu kushuka sana, ni udhaifu wa udhibiti wa utoroshaji wa zao la pareto. Zao la pareto linabebwa kwenye magunia, bodaboda wanabeba kutoka mashambani, ile *transaction* ambayo siyo ya kitaalamu inapunguza ubora wa pareto yetu kwa hiyo, *COPRA* wanapochukua zao hili jambo la kwanza liwe ni kudhibiti mianya ya kutorosha pareto kutoka mashambani. Wasipofanya hivyo, zao hili litabaki kuwa na sumu ndogo sana na hicho ndicho kinafanya pareto yetu inakuwa siyo bora.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni mgongano wa kiutendaji. *COPRA* wamekuja na wana mpango mzuri. Waweke utendaji mzuri kuanzia ngazi ya mkulima, kwa maana ya kuweka maafisa wa ugani, na kuboresha maeneo wanayofanyia kazi wakulima.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mengine kama unayo unamwandikia Waziri, anayapokea vilevile.

Mheshimiwa Nollo. Jiandae Mheshimiwa Dkt. Pindi.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, na mimi ninakushukuru kwa kunipa nafasi, ili niweze kuchangia hoja iliyopo mezani. Awali, lengo kubwa la Serikali lilikuwa ni kuifuta Bodi ya Pareto, ili kupunguza matumizi, mjadala mkubwa umefanywa na

kamati tukafikia kwamba, dhima isiwe kupunguza matumizi ya Serikali kwa kuifuta ile bodi ya pareto, lengo liwe ni kuboresha na kukuza zao la pareto.

Mheshimiwa Spika, sote tumekubaliana kwamba, ianzishwe kurugenzi ya pareto ndani ya ya *COPRA*, ambapo ndani ya *COPRA* yapo mazao takribani 100, ambayo inayasimamia. Sasa, kwa upekee wa pareto kuwe na kurugenzi, ambayo kwanza itafanya kazi ya kukuza zao lenyewe, kwa maana ya wakulima waongezeke, lakini vilevile kufanya tafiti juu ya ku-*scale up* zao la pareto na kuangalia *processing* ya ndani. Tuna kiwanda kimoja pale Mufindi, lakini ni cha muda mrefu na inawezekana kiko nyuma ya teknolojia.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kuangalia *the future and potential* ya zao la pareto, kwa maana kwamba, dunia sasa inaondoka kwenye matumizi ya kemikali. Inataka kwamba, tusitumie kemikali na badala yake twende kwenye *organic pesticides* na pareto ni *organic pesticides*. Sasa tuna nafasi kubwa ya sisi kwanza ndani ya Tanzania, baada ya kufanya utafiti, tuka-*process*. Dawa hizi zitatumika ndani ya nchi yetu na tayari tutakuwa tuna soko, kwanza ndani ya nchi, ambapo itakuwa kama ni *precursor*. Kwamba, mazao mengi sasa yatakuwa *treated organically*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni, dawa za mbu za kuchoma, zile za kufukuza mbu, ni pareto. Kuna watu wengi, hata rafiki zangu hapa wananiuliza, wanadhani pareto ni chakula! Pareto ni maua yenye sumu. Bahati mbaya hata Mheshimiwa Hokororo naye alikuwa ananiuliza! Kwa hiyo, pareto ni maua ambayo yanakuwa na sumu; sumu yake inatumika, kama nilivyoielezea hapo awali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo inasema, kufikia mwaka 2030 kuwe na uzalishaji wa tani 10,000 kutoka tani 4,000 za sasa. Jambo hili linahitaji nguvu na kujipanga, ili tuweze kufikia katika steji hiyo. Kwa sasa soko ghafi la pareto duniani ni karibu dola milioni 80 mpaka 130 kwa hiyo, sisi bado tuna nafasi kubwa kuanza kwenye ghafi, lakini tukija kwenye *processing* inaenda

karibu dola bilioni 1.2. Kwa hiyo, yote haya Serikali iangalie katika lengo la kuongeza uzalishaji wa pareto.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

Mheshimiwa Dkt. Pindi.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naanza kukupongeza wewe mwenyewe kwa kulisimamia vizuri zoezi ambalo tumemaliza hivi karibuni, la upigaji wa kura. Pia, ninaendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, Makamu wa Rais Mteule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri kwa kuleta muswada huu. Katika mjadala wa bajeti ya kilimo kipindi kilichopita, mwezi wa sita, Wabunge wengi walisema tuna bodi nyingi, tuangalie namna ya kuzi-*merge* hizi bodi. Mara baada ya kumaliza Bunge la bajeti, haraka sana Waziri ameleta; kwamba, Bodi ya Pareto sasa majukumu yake yaende kwenye mamlaka *(COPRA)* kwa hiyo, hii ni Serikali sikivu. Kwa kweli, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na ninampongeza sana na kumshukuru Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoona kwamba, zao la pareto ni miongoni mwa mazao muhimu sana. Hivisasa kilogramu moja ya pareto inaenda hela za Kitanzania zisizopungua shilingi 3,500. Eka moja unaweza ukazalisha kilogramu za maua zisizopungua takribani 450.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Njombe miaka ya nyuma ulikuwa ni miongoni mwa mikoa ambayo inazalisha sana pareto. Pareto hii maua yake yanatumika kwenye *cosmetic*, sabuni na *shampoo* kwa hiyo, soko lipo tena la kutosha. Hivyo, Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko, ambayo sasa wanachukua majukumu ya bodi ya pareto, pamoja na shughuli zao wahakikishe kwamba, zao hili la pareto wanalipa

kipaumbele. Tutaangalia takwimu za sasa na baada ya kuwapa mamlaka je, takwimu za uzalishaji zimeongezeka? *Export* imeongezeka? Fedha za nje zimeongezeka? Na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, nina imani sana na mamlaka ya udhibiti. Uwezo huu wanao.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mambo ambayo yameletwa katika muswada ni pamoja na Ibara ya 07 ya muswada, ambayo inaeleza wazi kabisa kwamba, watumishi watahamishwa kutoka bodi kwenda katika mamlaka ya *COPRA*. Sasa, ombi langu, ninaomba haki zao za kisheria zizingatiwe, ikiwa ni pamoja na masuala ya *NSSF, PSSF*, ushirikishwaji na wapewe majukumu. Watumishi hawa wasifike pale na kuwa *stranded* ikaonekana kwamba, wako wenye eneo lao la *COPRA* na wao wametoka huko waachwe! Wafanye kazi na wawashirikishe ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, Muswada huu wa kufuta Bodi ya Pareto ni mzuri; haya ni maelekezo na michango ya Wabunge. Wakasema kila zao lina bodi yake, sasa je, tunaweza tukaunganisha?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, usikivu huu, leo wameleta muswada wa kuunganisha haya majukumu, kama sisi wenyewe Wabunge tulivyosema. Hivyo ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nirejee kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja ya Muswada wa Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026. Ninaishukuru pia, Kamati ya Bunge chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Deo Mwanyika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango na maoni yenu. Tumeyapokea na tumeyazingatia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa, majukumu yote yaliyokuwa ya Bodi ya Pareto yatatekelezwa kwa ufanisi na *COPRA*. Mali, madeni na watumishi wa Bodi ya Pareto watahamishiwa *COPRA* na taasisi nyingine kwa kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026**

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4

Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 105(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025, ninaomba kutoa Taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria, Ibara kwa Ibara na kuukubali bila mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026 pamoja na marekebisho yake.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026 Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto na Kuweka Masharti Kuhusu Uhamisho wa Mali, Madeni, pamoja na Watumishi wa Bodi ya Pareto, Kuweka Masharti ya Mpito na Masuala Mengine Yanayohusiana na Hayo.**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umesomwa kwa mara ya tatu. Jukumu la Bunge limeishia hapa, sasa Muswada huu unapelekwa kwa Mheshimiwa Rais kwa idhini yake ili uweze kutumika.

Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri na Naibu wako, Kamati, Mwenyekiti na Wajumbe wako. Ninajua mlivutana, lakini hatimaye mmefikia mwafaka na mmeelewana; ndiyo kazi ya Bunge, ni mwafaka, Bunge siyo vita.

Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa *flexibility* ya Wizara yako. Kwa kuona maeneo ambayo Kamati imeyaona na kuyakubali, ili kusaidia wananchi katika maendeleo yao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo dogo. Wageni waliopo Bungeni mchana huu:-

Wageni watano wa Mheshimiwa Spika kutoka Baraza la Wawakilishi. Mheshimiwa Mahfoudh Abdallah Mohamed, Mwenyekiti wa *Baraza la Wawakilish*i *Sports Club*; Mheshimiwa Juma Thabit Kaponda, Katibu *Baraza la Wawakilishi Sports Club*; Mheshimiwa Ally Gulam**,** mwakilishi wa Naibu Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo. Mheshimiwa Salha Mwijuma, mwakilishi na Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi na Mheshimiwa Mwanaidi Kassim, mwakilishi wa Viti Maalumu. Karibuni sana na tunafurahi sana kuja kuungana na sisi kwenye bonanza la kesho. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno haya, ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.42 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 31 Agosti, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*